

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA
MHESHIMIWA STEPHEN WASIRA (MB.) KUHUSU MAKADIRIO YA
MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO CHAKULA NA
USHIRIKA KWA MWAKA 2007/2008**

I. UTANGULIZI

- 1.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili, na kukubali kupitisha makadirio ya Matumizi ya kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008.
- 2.** **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii kuungana na Watanzania kutoa pongozi za dhati kwa Mhe. Dkt. Asha Rose Migiro kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, mwanamke wa kwanza wa kiafrika. Uteuzi wake unatokana na utendaji wake uliotukuka katika nyadhifa zake mbalimbali alizowahi kuzishika hapa nchini, na sifa za Tanzania katika medani za Kimataifa tangu enzi za waasisi wa Taifa letu. Uteuzi wake ni sifa kubwa kwa Taifa letu. Tunamuahidi ushirikiano na kumtakia mafanikio makubwa katika wadhifa wake mpya. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Bernard Membe kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Namtakia mafanikio katika wadhifa huo mpya. Nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Batilda Burian, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge). Aidha, nawapongeza Waheshimiwa William Ngereja (Mb.) na Gaudence Kayombo (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri.
- 3.** **Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitoe pongozi kwa wenzetu waliochaguliwa kuwa wabunge wa bunge hili au wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Wabunge hao ni pamoja na Mheshimiwa Yusufu Rajab Makamba,

Mbunge wa kuteuliwa na Florence Essa Kyandesya Mbunge Viti Maalum. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mtutura Abdalla Mtutura kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru. Vile vile, nachukua fursa hii kuwapongeza Mhe. Sylvia Kate Kamba, Mhe. Dkt. Didas John Massaburi, Mhe. Dkt. Aman Walid Kabourou, Mhe. George Francis Nangale, Mhe. Sepetu Nassor, Mhe. Abdulla Ally Hassan Mwinyi, Mhe. Janet Mmari, Mhe. Dkt. Fortunatus Masha na Mhe. Gharib Billal, kwa kuchaguliwa kuwa wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

4. Mheshimiwa Spika, niruhusu nitumie fursa hii kwa mara nyingine kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Juma Jamaldin Akukweti, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge) aliyefariki tarehe 4 Januari, 2007 kutokana na ajali ya ndege iliyotokea huko Mbeya mwezi Desemba, 2006. Natoa pia salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, aliyekuwa Mbunge wa viti maalum, aliyefariki dunia tarehe 26 Juni, 2007. Aidha, natoa salaam za rambirambi kwa familia za marehemu Nathaniel Katinila, Theresia Nyantori na John Bendera, ambao walikuwa watumishi wa Serikali, waliofariki kutokana na ajali hiyo. Vile vile, kwa masikitiko makubwa, natoa salaam za rambirambi kwa familia za marehemu Hezron Ndono, Stephen Kazi na William Kasubi ambao walikuwa wajumbe wa Bodi ya Nyanza Cooperative Union (NCU), waliofariki katika ajali ya gari wakitokea Mwanza kuja Dodoma wakiwa kazini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na amsaidie Mama Modesta Bulugu, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa NCU, aliyepata majeraha katika ajali hiyo na ambaye anaendelea na matibabu katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili, apone haraka. Amina.

5. Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kutoa shukrani na pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi Mheshimiwa Gideon Cheyo (Mb.) na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano, na kwa mchango wao mkubwa, walioutoa katika kuboresha mipango na utekelezaji wa shughuli za kilimo. Kwa niaba yangu mwenyewe, Watendaji na Viongozi wenzangu, tunaahidi kuimarisha ushirikiano uliopo katika kuleta mapinduzi ya kilimo nchini.

6. Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wote wa Jimbo langu la Bunda, kwa ushirikiano na mchango wao mkubwa wanaoutoa katika kujiletea Maendeleo. Jimbo la Bunda lenye kata 12, linazo shule za Sekondari 20 za wananchi na shule 2 za binafsi. Mafanikio haya yametokana na kazi kubwa iliyofanywa na wananchi wenyewe. Aidha, nawapongeza viongozi wote wa Wilaya ya Bunda kwa mafanikio hayo. Kufuatia uchaguzi wa CCM katika ngazi ya Matawi na Kata nawapongeza wote waliochaguliwa na kuwatakia mafanikio katika kipindi chao chote cha uongozi.

7. Mheshimiwa Spika, hii ikiwa ni hotuba yangu ya kwanza tangu nilipohamishiwa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika mwishoni mwa mwaka jana, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Rais Jakaya M. Kikwete kwa imani yake anayoendelea kunipa, kwa kunateua kusimamia sekta hii muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Aidha, nampongeza kwa dhati Rais, Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Mohamed Shein na Waziri Mkuu kwa jinsi wanavyotumia muda wao mwingi kuhamasisha shughuli za kilimo.

8. Mheshimiwa Spika, pongezi za mwisho, nazitoa kwa Waziri Mkuu Mhe. Edward N. Lowassa (Mb.), Waziri wa Fedha Mhe. Zakia Hamdani Meghji (Mb.) na Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji Mhe. Alhaj Dkt. Juma A. Ngasongwa, kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa ufanuzi kuhusu hali ya uchumi na mwelekeo wa Bajeti ya Serikali, na kueleza kwa muhtasari

hali ya kilimo chetu ilivyo hivi sasa na mwelekeo kwa mwaka ujao. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge walotumia mijadala hiyo na kutoa michango mizuri sana kuhusiana na sekta ya kilimo. Wizara yangu imezingatia mawazo hayo yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

II. HALI YA KILIMO NA USHIRIKA NCHINI

9. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya kilimo nchini inaridhisha, ukitalia maanani kiwango chetu kidogo cha uwekezaji katika sekta ya kilimo. Pamoja na kiwango kidogo cha uwekezaji, kilimo kimeendelea kuwa sekta muhimili, yenye mchango mkubwa katika pato la Taifa. Kwa mwaka 2006, mchango wa kilimo ulikuwa asilimia 44.7, ukilinganisha na sekta nyingine kwa pamoja, ambazo zimechangia asilimia 55.3 ya pato la Taifa. Sekta ndogo ya mazao peke yake ilichangia asilimia 33.4 ya pato la Taifa katika mwaka 2006. Takwimu hizi zinathibitisha kuwa hatuna njia ya mkato ya kuinua kipato cha wananchi walio wengi na kufikia azma ya maisha bora kwa kila Mtanzania bila ya kuleta mapinduzi katika kilimo. Nitaeleza hatua za muda mfupi na wa kati za kutuelekeza katika kuleta mapinduzi ya kilimo, nitakapozungumzia makusudio ya Wizara yangu katika mpango wa mwaka 2007/08. Sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 4.1 mwaka 2006 ikilinganishwa na asilimia 5.1 mwaka 2005. Kushuka huku kwa ukuaji wa Sekta mwaka 2006, kulitokana hasa na ukame ulioikumba sehemu kubwa ya nchi yetu msimu wa 2005/2006.

Hali ya Chakula Mwaka 2006/2007

10. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 upatikanaji wa chakula kwa ujumla, ukilinganishwa na mahitaji, ulikuwa mzuri kutoptana na mvua za vuli na masika kunyesha kwa mtawanyiko mzuri. Kutoptana na hali hiyo, uzalishaji wa mazao ya chakula katika mwaka 2005/2006 ulikuwa tani milioni 10.95. Kati ya hizo, tani milioni 5.30 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani

milioni 5.67 mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula yalikuwa tani milioni 9.75 na kufanya Taifa kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 112. Hata hivyo, baadhi ya maeneo katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Shinyanga na Singida yalikuwa na upungufu wa chakula uliosababishwa na upungufu wa mvua.

11. Mheshimiwa Spika, tathmini ya kina ya hali ya chakula iliyofanywa na Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo mwezi wa Agosti, 2006 ilibaini kwamba watu 651,655 walivuna chini ya asilimia 30 ya mahitaji yao ya chakula, hivyo walihitaji chakula cha msaada. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani ilisambaza jumla ya tani 10,500 kwenye maeneo yaliyokuwa na upungufu wa chakula.

Matarajio ya Upatikanaji wa chakula 2007/2008

12. Mheshimiwa Spika, matokeo ya tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini katika msimu wa kilimo wa 2006/2007 yanaonyesha kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani milioni 11.02 zikiwemo tani milioni 5.85 za mazao ya nafaka na tani milioni 5.17 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2007/2008 yamekisiwa kufikia tani milioni 10.09. Kwa hiyo, inatarajiwa kuwa Taifa litajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 109.

13. Mheshimiwa Spika, tathmini hiyo pia imeonyesha kwamba Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Mtwara, Kigoma na Lindi itajitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada. Mikoa ya Morogoro, Manyara, Kagera, Dodoma, Mwanza, Tanga, Pwani, Mara na Shinyanga itajitosheleza kwa chakula na haitakuwa na ziada. Mikoa ya Tabora, Singida, Kilimanjaro, Arusha na Dar es

Salaam itakuwa na upungufu wa chakula kwa viwango tofauti. Upungufu wa chakula katika mikoa hiyo ulitokana na mvua nyingi na kutuama maji katika miezi ya Desemba, 2006 na Januari, 2007 na kuzuia kazi za kilimo katika baadhi ya maeneo ya mikoa hiyo. Aidha, upungufu wa chakula kwa mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka umetokana na kuchelewa kuanza kunyesha na kukatika mapema kwa mvua za masika.

14. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza, Serikali itachukua hatua zifuatazo:-

- Kufanya tathmini ya kina kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine katika maeneo yenye upungufu wa chakula mwezi Agosti 2007. Lengo ni kubaini kaya zitakazokuwa na upungufu wa chakula na hatua za kuchukuliwa;
- Kuimarisha uwezo wa Akiba ya Taifa ya Chakula (*Strategic Grain Reserve-SGR*) wa kununua na kuhifadhi tani 27,500 za nafaka katika mikoa yenye ziada ya chakula;
- Kuwahimiza wananchi waliopata mavuno mazuri ya chakula katika msimu wa 2006/2007 kujiwekea akiba ya chakula ya kukidhi angalau mahitaji ya kaya hadi kufikia mavuno ya msimu wa 2007/2008;
- Kuwahimiza wafanyabiashara kununua chakula kutoka kwenye maeneo yenye ziada na kukiiza kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula kwanza kabla ya kufikiria kukiiza nje ya nchi;
- Kuwahimiza wananchi wanaotegemea mifugo kwa ajili ya kipato chao, kuuza baadhi ya mifugo wakati huu ambapo ina hali nzuri na bei ziko juu ili wajinunulie na kuhifadhi chakula cha kutosha mahitaji yao hadi msimu ujao;
- Kuwahamasisha wananchi wengine wanaotegemea kipato kutokana na shughuli zingine ambazo si za kilimo cha mazao ya chakula, kununua

chakula cha kutosha mahitaji yao wakati wa kipindi cha mavuno ambapo bei za vyakula zinakuwa nafuu;

- Kuwahimiza wananchi kutegemea zaidi vyakula vinavyopatikana kwa wingi katika maeneo wanayoishi;
- Kuendelea kuratibu kwa karibu hali ya chakula nchini na kuchukua hatua zinazostahili kulingana na hali inayojitokeza.

Hali ya Chakula Nchi za Jirani

15. Mheshimiwa Spika, taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) ya Aprili, 2007 kuhusu matarajio ya uzalishaji wa mazao ya chakula Duniani inaonyesha kuwa nchi za Kusini mwa Afrika, hususan Afrika ya Kusini, Lesotho, Swaziland, Namibia, Botswana na Zimbabwe zitakuwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame. Aidha, nchi za Zambia, Msumbiji na Madagascar mvua kubwa zilizonyesha kuanzia Januari hadi Machi, 2007 zilisababisha mafuriko makubwa yaliyoharibu miundombinu, mazao mashambani na kusababisha kushuka kwa uzalishaji katika baadhi ya maeneo. Nchi ya Malawi inatarajiwa kuwa na mavuno mengi kutokana na kupata mvua za kutosha zenyenye mtawanyiko mzuri. Nchi ya Uganda itakuwa na hali nzuri ya chakula isipokuwa maeneo ya Kaskazini. Nchi za Kenya, Burundi na Rwanda pamoja na kupata mvua nzuri na mavuno mazuri katika baadhi ya maeneo, zitaendelea kuwa na upungufu wa chakula. Hali ya chakula katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (*DRC*), inaweza kuendelea kuwa mbaya kwa sababu ya vita.

16. Mheshimiwa Spika, upungufu wa chakula katika nchi jirani unaweza kuathiri upatikanaji wa chakula nchini kutokana na biashara za mazao ya chakula mipakani. Biashara ya mazao hayo hufanyika sana katika mipaka ya Tanzania na Kenya, Malawi, Zambia, Rwanda, Burundi, Kongo na Uganda. Hivyo, Wizara itashirikiana na Mikoa husika kuwahamasisha wananchi

kuhifadhi mazao ya chakula kulingana na mahitaji ya kaya zao na kuuza ziada ili taifa linufaika na fursa ya masoko yatakayotokana na uhaba wa chakula katika nchi hizo.

Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara

17. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa chai, kahawa, korosho na mkonge uliongezeka kwa kati ya asilimia 11 na 42. Ongezeko hilo limechangiwa na ufuluaji na upanuzi wa mashamba, matumizi ya miche bora yenyе tija kubwa zaidi na upatikanaji wa mvua katika maeneo yanayozalisha mazao hayo. Uzalishaji wa mazao ya pamba na sukari ulishuka kutokana na hali ya ukame ulioyakumba maeneo yanakozalishwa mazao hayo. Uzalishaji wa pareto ulishuka kutokana na kuanza kwa zoezi la kung'oa pareto ya zamani ili kupanda pareto mpya yenyе tija zaidi. Aidha, uzalishaji wa sukari ulishuka kutokana na ukame uliotokea katika msimu wa 2005/2006 na mvua nyingi zilizokwamisha uvunaji msimu wa 2006/2007. Uzalishaji wa mazao makuu ya biashara kwa msimu wa 2006/2007 ulikuwa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.**

Jedwali Na.1 Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara

Zao	Uzalishaji (Tani)		Badiliko (%)
	2005/06	2006/07	
Kahawa	34,334	48,869	42.3
Tumbaku	56,463	65,299	15.7
Chai	30,000	34,446	14.8
Pareto	2,800	1,500	-46.4
Mkonge	27,794	30,934	11.3
Korosho	77,158	92,232	19.5
Pamba	376,591	130,565	-65.3
Sukari	263,317	192,535	-26.9

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

i. Kahawa

18. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa kahawa msimu wa 2006/2007 uliongezeka kwa asilimia 42.3 ambapo tani 48,869 zilizalishwa ukilinganisha na tani 34,334 zilizozalishwa msimu 2005/2006. Ongezeko hilo lilitokana na miche bora yenyе ukinzani dhidi ya magonjwa ya chule buni (*Coffee Berry Disease – CBD*) na kutu ya majani (*Coffee Leaf Rust - CLR*) na wadudu waharibifu iliyopandwa miaka ya nyuma, wakulima kuzingatia mafunzo ya kilimo bora na upatikanaji wa bei nzuri ya kahawa. Lengo la kuzalisha tani 55,000 halikufikiwa kutokana na baadhi ya wakulima kuendelea kutunza mibuni iliozeeka na ambayo haina ukinzani dhidi ya magonjwa ya chule buni na kutu ya majani na wadudu waharibifu, tija ndogo kutokana na matumizi madogo ya pembejeo, matumizi madogo ya umwagiliaji maji katika kilimo cha kahawa na huduma duni za ugani.

ii. Chai

19. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2006/2007 uzalishaji wa chai ulikuwa tani 34,446 sawa na ongezeko la asilimia 14.8 ya uzalishaji wa tani 30,000 msimu wa 2005/2006. Kiwango hiki cha uzalishaji kimetokana na ufufuaji wa mashamba ya wakulima wadogo wa chai katika wilaya za Njombe, Bukoba na Muleba, upanuzi wa kilimo cha chai wilaya za Njombe, Mufindi na Kilolo na upanuzi katika maeneo mapya ya wilaya za Ludewa na Tarime. Sababu nyingine ni mafunzo ya mbinu za kilimo bora cha chai yaliyotolewa kwa wakulima na hivyo kuongeza tija, upatikanaji wa miche bora iliyosambazwa kwa wakulima na bei nzuri ya majani ya chai waliyopata wakulima.

iii. Korosho

20. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2006/2007 uzalishaji wa korosho uliongezeka kwa asilimia 19.5 kutoka tani 77,158 zilizozalishwa katika msimu wa 2005/2006 hadi tani 92,232. Sababu za kuongeza kwa uzalishaji huo ni

juhudii za wakulima kuitikia wito wa serikali wa utunzaji wa mashamba ya mikorosho, upatikanaji wa madawa ya korosho yenyeye ruzuku na usimamizi wa karibu kuanzia ngazi ya kijiji, wilaya na mkoa katika maeneo yote yanayolima korosho. Lengo la kuzalisha tani 115,000 halikufikiwa kutokana na upungufu wa mvua, ugonjwa wa ubwiri unga, mikorosho mingi kuzeeka, kutozingatiwa kwa kanuni za kilimo bora cha korosho, wakulima wengi kutotumia miche bora ya korosho na ukosefu wa mitaji ya kuendeleza zao hilo.

iv. Pamba

21. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2006/2007 uzalishaji wa pamba ulikuwa tani 127,600, sawa na marobota 245,000, ukilinganisha na tani 363,229 msimu wa 2005/2006. Lengo la kuzalisha tani 200,000 halikufikiwa kutokana na ukosefu wa mvua za kutosha katika maeneo makuu ya uzalishaji wa pamba, matumizi madogo ya viuatilifu na yasiyozingatia viwango vilivyopendekezwa na wataalam na kutokuzingatiwa kwa kanuni za kilimo bora na cha zao hilo.

v. Tumbaku

22. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa tumbaku katika msimu wa 2006/2007 ulikuwa tani 65,299 ukilinganishwa na tani 56,463 zilizozalishwa msimu wa 2005/2006, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Ongezeko la uzalishaji lilitokana na usajili wa wakulima uliorahisisha usimamizi wa kanuni za uzalishaji na upangaji wa madaraja. Aidha, kuongezeka kwa matumizi ya mbegu bora na mbolea yenyeye ruzuku, kuimarisha huduma za ugani na upatikanaji wa soko la uhakika kwa utaratibu wa kilimo cha mkataba kulichangia ongezeko la uzalishaji wa zao hilo. Ili kukabiliana na upatikanaji wa kuni za kukaushia tumbaku na kupunguza uharibifu wa mazingira unaochangiwa na ukataji wa miti, jumla ya miti milioni 7.2 ilipandwa ikilinganishwa na lengo la kupanda miti milioni 8.0, sawa na asilimia 90 ya lengo.

vi. Sukari

23. Mheshimiwa Spika, katika msimu 2006/2007 uzalishaji wa sukari
nchini ulikuwa tani 192,535 sawa na asilimia 61.7 ya lengo la uzalishaji wa tani 312,000. Uzalishaji huo ni sawa na upungufu wa asilimia 26.9 ukilinganisha na uzalishaji katika msimu wa 2005/2006 ambapo tani 263,317 zilizalishwa. Kushuka kwa uzalishaji kulitokana na ukame wa msimu 2005/2006 ulioathiri upandaji na ustawi wa miwa na kuwepo kwa mvua nyingi kuliko wastani katika msimu wa 2006/2007 iliyoathiri usombaji wa miwa kutoka mashambani kwenda viwandani, hususan vya Kilombero na Mtibwa na hivyo kufanya usindikaji kusimama mwezi Desemba, 2006 kwa ukosefu wa miwa. Sababu nyinegine ilikuwa ni matatizo ya mtambo wa *boiler* na *turbo alternator set* na migomo ya wafanyakazi katika kiwanda cha TPC uliosababisha wafanyakazi 168 kuachishwa kazi. Aidha, kiwanda cha TPC kilipata dosari ya kuunguliwa na kifaa cha kupakia miwa chenye thamani ya shilingi milioni 190 na miwa ya thamani ya shilingi milioni 137 kuunguzwa.

vii. Pareto

24. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa pareto ulishuka kwa asilimia 46.4
kutoka tani 2,800 msimu 2005/2006 hadi tani 1,600 msimu 2006/2007. Kushuka kwa uzalishaji kulitokana na zoezi la kubadilisha mashamba kwa kung'oa miche ya zamani na kupanda miche bora ya vikonyo (*clonal materials*) yenyе tija kubwa na sumu nyingi iliyozalishwa na kituo cha utafiti cha Uyole, Mbeya. Pamoja na kushuka kwa uzalishaji, upandaji wa ina mpya za miche ulichangia kuongezeka kwa tija tija iliongezeka kutoka kilo 250 kwa hekta msimu 2005/2006 hadi kilo 450 kwa hekta moja msimu 2006/2007. Ubora wa sumu uliongezeka kutoka asilimia 0.8 hadi asilimia 1.3.

viii. Mkonge

25. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa katani uliongezeka kutoka tani
27,794 msimu 2005/2006 hadi tani 30,934 msimu 2006/2007, sawa na ongezeko

la asilimia 11.3. Ongezeko hilo lilitokana na kupanuliwa kwa maeneo yanayozalisha mkonge, kuhusisha wakulima wadogo chini ya utaratibu wa kilimo cha mkataba. Aidha, uzalishaji wa mkonge umekuwa ukiongezeka kutokana na mahitaji ya bidhaa za mkonge duniani kwa matumizi mbalimbali ambayo ni pamoja na nishati, ujenzi, karatasi na mbolea. Matumizi hayo, yamesababisha ongezeko la bei ya katani ambayo imehamasisha wakulima. Kwa mfano, bei ya daraja la tatu (UG) kwa tani imeongezeka kutoka dola za Kimarekani 760 kwa tani mwaka 2005 hadi dola 900 mwaka 2007.

Uzalishaji wa mazao Mapya

26. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuhimiza kilimo cha mazao mapya yenye thamani kubwa na soko la uhakika. Mazao hayo ni pamoja na vanilla, mazao ya mboga, viungo kama iliki, mdalasini, tangawizi na pilipili manga. Aidha, Wizara ilihimiza kilimo cha miembe, mananasi, migomba, michungwa na miparachichi. Wastani wa vipando bora 100,000 vya mazao mbalimbali ya bustani vilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima. Wizara iliwezesha upatikanaji wa tani nne za mbegu za jatrofa kwa ajili ya mashamba ya mfano ya uzalishaji wa zao hilo kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya, JKT na wakulima binafsi. Kiasi hicho cha mbegu kiliotesha katika jumla ya hekta 700. Mashamba hayo yatakuwa ni vyanzo vya mbegu za zao hilo na vituo vya kufundishia wakulima na wataalam kuhusu zao hilo. Vilevile, Wizara imekuwa ikishirikiana na Idara ya Magereza katika kuzalisha vipando bora vya mihogo kama mbinu ya kuendeleza zao hili nchini ambapo jumla ya vipando milioni kumi na moja vilizalishwa.

Hali ya Ushirika

27. Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada za serikali na za wadau mbalimbali za kufufua, kuanzisha na kuimarisha ushirika nchini, idadi ya vyama vya ushirika iliongezeka kutoka 5,832 mwaka 2005/2006 hadi 7,299 mwaka 2006/2007, sawa na ongezeko la asilimia 25. Katika kipindi hicho ongezeko kubwa lilikuwa katika Vyama vya Ushirika wa

Akiba na Mikopo (SACCOS) ambapo viliongezeka kutoka vyama 2,028 hadi 3,469, sawa na ongezeko la asilimia 71 na idadi ya wanachama katika vyama hivyo iliongezeka kutoka 291,368 hadi 590,163, sawa na ongezeko la asilimia 102.5. Mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kutoka shilingi bilioni 65.7 hadi shilingi bilioni 116.7, sawa na ongezeko la asilimia 75.2. Mikopo hiyo ilitolewa kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, biashara ndogo ndogo, ujenzi wa nyumba, elimu na tiba. Hata hivyo, baadhi ya vyama vinakabiliwa na uendeshaji mbaya, uwezo mdogo wa kushindana kibiashara na mtaji mdogo.

III. MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA 2006/2007

Mapato

28. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 741,577,000 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato hususan ushuru wa ukaguzi wa mazao. Hadi mwezi Juni, 2007, kiasi cha shilingi 747,587,762.9 sawa na asilimia 100.8 ya makadirio yaliyokusanywa.

Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2006/2007

29. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 121.6 na kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 75.78 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 45.812 kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo.

Matumizi ya Kawaida

30. Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 26 Juni, 2007, Wizara ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya shilingi 58,532,564,701 sawa na asilimia

77.2 ya kiasi kilichoidhinishwa. Matumizi hadi sasa ni shilingi 57,099,827,256.16 sawa na asilimia 97.6 ya kiasi kilichotolewa.

Matumizi ya Maendeleo

31. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 45.812 kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi bilioni 8.353 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 37.458 ni fedha za kigeni. Fedha za ndani zilizotolewa ni shilingi bilioni 5.91 sawa na asilimia 70.7 ya fedha zilizoidhinishwa. Fedha za nje zilizotolewa ni shilingi bilioni 23.37 na matumizi shilingi bilioni 22.1 sawa na asilimia 94.57 ya kiasi kilichotolewa. Kutokupatikana kwa fedha zote zilizoidhinishwa kuliathiri utekelezaji wa baadhi ya kazi zilizopangwa.

IV. TAARIFA YA UTEKELEZAJI MWAKA 2006/2007

32. Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea kutekeleza majukumu yake muhimu ambayo ni pamoja na kuimarisha huduma muhimu za kiufundi na kitaalam kwa wakulima, kuratibu hali ya chakula nchini, kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya kuendeleza kilimo, kudhibiti mlipuko wa magonjwa, wadudu na wanyama waharibifu pamoja na kuimarisha utawala bora. Majukumu yote ya Wizara yalitekelezwa chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme –ASDP*).

33. Mwaka 2006/2007, ulikuwa ni wa kwanza kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP). Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project- PADEP*), Mradi wa Uwekezaji Katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agricultural Investment Project-DASIP*) pamoja na

Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Program Support-ASPS*) ni sehemu ya utekelezaji wa ASDP. Ili ASDP iweze kutekelezwa kwa ufanisi, katika mwaka 2006/2007 Wizara ilifanya maandalizi yafuatayo:

Kukamilisha taratibu za kuwezesha utekelezaji wa Programu kuanza

- Uzinduzi wa programu ulifanyika Julai 2006 na semina zilitolewa kwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya, Wakuu wa Wilaya, pamoja na Sekta binafsi na asasi zisizo za kiserikali.
- Miongozo ya kupanga, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) ilitayarishwa na kupelekwa kwa watendaji wa Halmashauri zote nchini.

Kuzijengea halmashauri za Wilaya uwezo wa kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs).

- Timu za Wawezeshaji za Wilaya (*District Facilitation Teams*) katika halmashauri zote zilipata mafunzo ya namna ya kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya zao. Wataalam 882 wa Wilaya walipata mafunzo hayo. Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya 121 iliandaliwa.

Kuandaa utaratibu wa kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa ASDP

- Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini (*M&E Framework*) unaendelea kuandaliwa na kamati ya ufuatiliaji na tathmini inayojumuisha Wizara za Sekta ya Kilimo.

34. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2006/2007 Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:

Kuhakikisha Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

35. **Mheshimiwa Spika**, makadirio ya mahitaji ya mbolea za aina mbalimbali katika msimu wa 2006/07 yalikuwa tani 385,000. Hata hivyo, upatikanaji ulikuwa tani 284,924.67, ambazo ni sawa na asilimia 74 ya mahitaji. Kati ya hizo, tani 108,703 zilikuwa ni zenyeye ruzuku. Katika mwaka 2006/2007, Wizara ilitengewa shilingi bilioni 21. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.5 zilihamishiwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa ajili ya kutoa ruzuku ya madawa ya majosho ya mifugo. Hivyo, fedha ya ruzuku ya mbolea na mbegu bora zilizobaki zilikuwa shilingi bilioni 19.5: shilingi bilioni 16.5 zilitosha kufidia tani 108,703 za mbolea, shilingi bilioni 2.0 kufidia tani 3,000 za mbegu bora na shilingi bilioni 1 madawa ya korosho. Hadi Mei 2007 tani 88,407 za mbolea na tani 814 za mbegu bora za mahindi na mtama zilikuwa zimeuzwa kwa wakulima. Aidha, mahitaji ya mbegu bora yalikisiwa kuwa tani 30,000 lakini upatikanaji ulikuwa tani 12,119.8 tu.

Mfuko wa Pembejeo

36. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2006/2007, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulitengewa jumla ya Shilingi bilioni 3.5. Hadi Mei, 2007 shilingi bilioni 2.18 zilitolewa kwa ajili ya mikopo mbalimbali ya pembejeo na zana kupitia SACCOS, Halmashauri na wakulima. Aidha, Mfuko ulikusanya marejesho ya mikopo iliyotolewa misimu iliyopita yenye thamani ya shilingi bilioni 2.38 na kufanya jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mikopo kufikia shilingi bilioni 4.56. Mfuko ultoa mikopo ya pembejeo za kilimo na mifugo kama ifuatavyo; (i) Ununuzi wa matrekta makubwa mapya 81 yenye thamani ya shilingi 2,490,139,119; (ii) Ununuzi wa matrekta madogo mapya (Power tillers) 51 yenye thamani ya shilingi 255,000,000; (iii) Ukarabati wa matrekta matano kwa thamani ya shilingi 17,425,000 na (iv) Ununuzi wa

pembejeo za kilimo na mifugo zenyenye thamani ya shilingi 1,804,751,800 ambazo ni: Mbolea tani 2,729, Mbegu bora tani 37, Madawa ya mifugo lita 3,301, vyakula vya mifugo tani 40, madawa ya mimea lita 6,931, zana ndogo ndogo 19,100 na vifungashio marobota 16.

Kuimarisha Huduma za Kilimo

Huduma za ugani

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/07, Wizara iliendelea kusimamia utoaji wa ushauri wa kitaalam katika halmashauri na asasi nyingine. Wizara kwa kushirikiana na halmashauri ilitoa mafunzo ya Shamba Darasa kwa maafisa ugani ngazi ya wilaya 147 na kwa wakulima 100, ili dhana hiyo itumike kueneza kanuni za kilimo bora. Maafisa ugani waliopata mafunzo hayo walitoka wilaya za mikoa ya Lindi, Mtwara, Dodoma, Singida, Tanga, Pwani, Morogoro, Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Arusha, Manyara, Mara, Kagera, Kigoma, Tabora, Mwanza na Shinyanga. Wakulima waliopata mafunzo walitoka wilaya za Mbeya vijijini, Rungwe, Songea, Namtumbo, Arusha Manispaa, Babati, Morogoro vijijini, Mvomero, Kongwa na Dodoma vijijini. Aidha, Wizara iliratibu maandalizi ya maonyesho ya siku ya wakulima Nane nane na ya Siku ya Chakula Duniani.

38. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI Wizara ilifanya uchambuzi wa hali ya huduma za ugani nchini ili kuziboresha. Uchambuzi huo umeonyesha kuwa kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa ugani. Wakati mahitaji ni zaidi ya wataalam 15,000, waliopo ni 3,379 tu, hivyo kuna upungufu wa wataalam 11,703. Aidha, imebainika kwamba kuna uhaba wa vitendea kazi vya aina mbalimbali na nyumba za kuishi wataalam vijijini. Kutokana na uchambuzi huo, Wizara imetayarisha mpango wa miaka minne wa kuimarisha huduma hizo ambao utekelezaji wake utaanza mwaka 2007/08.

Mpango huo unalenga kuhakikisha vijiji, kata na tarafa zote nchini zinapata wataalam wa kilimo wa kutosha ili utaalam umfikie mkulima.

Utafiti wa Kilimo

39. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/07 shughuli za utafiti wa mazao ya Kilimo ziliendelea kutekelezwa katika kanda zote 7 za utafiti wa kilimo zenyenye jumla ya vituo 17 kwa lengo la kupata mbegu zenyenye sifa za kutoa mavuno mengi kwa eneo, zinazostahimili ukame, magonjwa na visumbufu vyatya mimea pamoja na kupendwa na walaji. Aina 16 za mbegu za korosho zilitolewa na kituo cha utafiti cha Naliendele ambazo ni: AC1, AC4, AC4/17, AC10, AC10/129, AC10/220, AC14, AC22, AC34, AC43, AZA2, AZA17, AZA17/179, AZA17/156, AZA17/158, AC4/285. Aidha, mbegu ya ngano itwayo Lumbesa ilitolewa na kituo cha utafiti cha Selian, Arusha. Mbegu mama za jamii ya nafaka, mikunde na mafuta zilizalishwa katika vituo mbalimbali vyatya utafiti. Taasisi za Utafiti za TaCRI (kahawa) na TRIT (chai) na vikundi vyatya wakulima vilizalisha miche bora ya kahawa 2,850,000 na miche bora 24,840,183 ya chai. Idadi ya miche ya chai ilisambazwa kama ifuatavyo, Mufindi (10,637,485), Njombe (9,863,031), Rungwe (241,451), Muheza (2,099,701), Korogwe (513,500) na Lushoto (1,485,000).

40. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/07, Wizara kupitia Mradi Shirikishi wa Kilimo na Uwezeshaji (PADEP) ilikamilisha ukarabati mkubwa wa maabara za udongo za Mlingano, Uyole, UKiriguru na Seliani. Maabara hizo zitatumika katika kuchunguza sampuli za udongo na kushauri aina na kiasi cha mbolea kinachopaswa kuwekwa kwenye mazao. Kwa mfano maabara ya Mlingano ina uwezo wa kuchunguza sampuli 5,000 kwa mwaka badala ya sampuli 2,000 hapo awali. Aidha, mwaka 2006/07, Wizara kupitia kituo cha Utafiti cha Mlingano kwa kutumia technologia ya GIS kimeweza kutengeneza

ramani za udongo kwa nchi nzima na wilaya zote. Pia ramani za ekolojia zilitayarishwa pamoja na ramani zinazoonyesha mazao yanayofaa kulimwa katika kila wilaya. Ramani hizo zimewekwa kwenye tovuti (website) ya Wizara (www.agriculture.go.tz). Pia ramani hizo zimewekwa kwenye CD na kusambazwa kwenye wilaya zote.

Udhibiti wa Visumbufo vya Mimea na Mazao

41. Mheshimiwa Spika, Ili kukabiliana na milipuko ya visumbufo vya mimea na mazao, katika mwaka 2006/2007 Wizara ilitekeleza yafuatayo;

- Ilidhibiti milipuko ya panya katika viji 622 vya Wilaya za Mvomero, Morogoro Vijijini, Morogoro Mjini, Ulanga, Kilombero, Bagamoyo, Mkuranga, Kibaha Mjini, Kisarawe, Rufiji, Muheza, Handeni, Korogwe, Pangani, Kilindi, Lindi Vijijini, Liwale, Nachingwea, Ruangwa, Kilwa, Moshi Vijijini, Hai, Monduli, Kinondoni, Temeke, Nzega na Masasi. Kilo 3,606.11 za sumu ya panya zilitumika. Aidha, wakulima 67,670 walipata mafunzo ya kudhibiti panya katika wilaya hizo;
- Ilidhibiti kwelea kwelea katika mikoa ya Morogoro, Singida, Shinyanga, Mwanza, Kilimanjaro na Dodoma. Ndege zaidi ya milioni 95 waliangamizwa na lita 4,210 za viuatilifu zilitumika. Ndege hao wasingedhibitiwa, wangeweza kusababisha uharibifu wa karibu tani 955 za nafaka kwa siku;
- Ilidhibiti nzige wekundu kwenye mazalio yao ya asili katika mbuga za Malagarasi, Ziwa Rukwa, Iku/Katavi, Wembere na Bahi. Nzige hao walikuwa kwenye eneo lenye jumla ya hekta 16,580. Jumla ya lita 7,895 za viuatilifu;

- Ilitoa mafunzo ya kutabiri na kudhibiti viwavijeshi kwa mabwana shamba 871, wakulima 232 na wahudumu wa mitego 34 katika mikoa ya Morogoro, Lindi, Mtwara, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.
- Wataalamu 54 na wakulima kutoka mikoa ya Kigoma, Kagera, Singida, Mtwara, Morogoro, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza, Kagera na Mara walipatiwa mafunzo ya matumizi ya udhibiti husishi;
- Ilidhibiti ugonjwa wa mnyauko wa migomba katika mikoa ya Kagera na Mara kwa kungo'a migomba 40,644 iliyokuwa imeathirika na ugonjwa huo.
- Mafunzo ya udhibiti wa nzi wa matunda yalitolewa kwa wataalam 93 wa kilimo na wakulima 800 wa wilaya za mikoa ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Pwani na Dar es Salaam;
- Jumla ya tani 259,831 za mazao mbalimbali zilikaguliwa na kusafirishwa nchi za nje na tani 630,209 ziliingizwa nchini ambapo vyeti 3,874 vya usafi wa mazao na vibali 257 vya kuingiza mazao nchini vilitolewa;
- Wadudu 620,000 wa kudhibiti kidung'ata wa mihogo walizalishwa na kusambazwa. Aidha, mbawakavu milioni 6.9 ambao hudhibiti gugumaji walizalishwa na kusambazwa katika maeneo mbalimbali katika Ziwa Viktoria. Vilevile, wadudu 810,000 maadui wa funza wa mabua na nondo wa kabichi walizalishwa na kusambaza kwenye mikoa ya Tanga, Iringa, Morogoro, Dodoma, Singida, Arusha na Kilimanjaro.

Usalama wa Chakula

Ukusanyaji wa Takwimu za Mvua na Hali ya Chakula

42. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, mfumo wa ukusanyaji takwimu na taarifa za hali ya chakula nchini uliboreshwu kwa kutoa mafunzo ya ufuatiliaji wa hali ya mazao mashambani na hali ya chakula kwa wataalam wa ugani katika Halmashauri za Wilaya na Miji katika Mikoa yote. Mafunzo ya mifumo ya ukusanyaji wa taarifa za mvua na mazao mashambani kwa wapima mvua kutoka katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga na Tanga yalitolewa. Aidha, ukusanyaji wa taarifa za mvua, uzalishaji wa mazao na mwenendo wa hali ya chakula nchini ulifanyika. Vilevile, kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Taasisi ya Chakula na Lishe Wizara iliandaa mwongozo wa kuratibu akiba ya chakula. Mwongozo huo utatumwiwa na Halmashauri katika kuratibu akiba ya chakula katika ngazi ya kaya. Wizara pia iliandaa rasimu ya Mkakati wa Usalama wa Chakula nchini.

Hifadhi ya chakula na Usindikaji

43. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara ilifanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kuhusu teknolojia za hifadhi, usindikaji na matumizi ya mazao mbalimbali ya chakula na kutoa mafunzo katika mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa na Mtwara. Mafunzo hayo yalilenga kupanua matumizi ya teknolojia hizo na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna. Wizara pia ilichapisha na kusambaza miongozo ya utayarishaji na matumizi ya mazao ya muhogo, mtama, mbogamboga na matunda na ilianza kuandaa mwongozo wa uchanganyaji wa mazao ya muhogo na mtama na nafaka nyingine ili kupanua matumizi ya mazao hayo.

44. Mheshimiwa Spika, mojawapo ya mkakati wa Serikali wa kupanua usindikaji wa mazao ya chakula nchini ni kuwapatia wawekezaji taarifa kuhusu maeneo yenye uwezo wa kuzalisha mazao mbalimbali, aina ya mazao, kiasi

kinachozalishwa, miundombinu iliyopo, viwanda vya usindikaji vilivyopo na uwezo wake. Taarifa hizo husaidia na huhamasisha wawekezaji kufanya maamuzi ya kuwekeza katika usindikaji wa mazao. Katika mwaka 2006/2007 Wizara iliendelea kuorodhesha viwanda vya usindikaji wa mazao ya chakula na uwezo wa kila kiwanda kukusanya takwimu za uzalishaji na idadi ya maghala ya kuhifadhi mazao ya chakula na uwezo wake vilivyopo nchini.

Akiba ya Taifa ya Chakula

45. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Akiba ya Taifa ya Chakula (SGR) ilinunua jumla ya tani 122, 098 zenyе thamani ya shilingi milioni 24,419.40. Kati ya hizo, tani 92,098 za mahindi zenyе thamani ya shilingi milioni 18,419.50 zilinunuliwa kutoka kwa wakulima wa hapa nchini na tani 30,000 zenyе thamani ya shilingi milioni 10,586 zilinunuliwa kutoka nje ya nchi. Ununuzi huo pamoja na akiba ya mwanzo wa mwaka ya tani 6,570.465 yanafanya SGR kuwa na jumla ya tani 128,668 za mahindi katika maghala yake. Aidha, Akiba ya Taifa ya Chakula ilinunua mtama jumla ya tani 2,831.325.

Umwagiliaji Maji Mashambani

46. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara ililenga kuendeleza hekta 10,000 za umwagiliaji. Eneo lililoendelezwa ni hekta 9,557 katika maeneo mbalimbali. Aidha, Wizara kwa kupitia kanda za umwagiliaji imefanya upembuzi yakinifu wa awali na usanifu wa skimu 62 zenyе jumla ya hekta 110,675 (**Kiambatisho Na. 1**) na mabwawa manne (4) yenyе kutosheleza eneo la umwagiliaji la hekta 780, mabwawa hayo ni Ulyanyama (Sikonge) hekta 500, Mawemairo (Babati) hekta 100, Idodoma (Mpwapwa) hekta 100 na Migungani (Bunda) hekta 80. Kazi zingine zilizotekelizwa ni ujenzi wa mabwawa mawili (2) yenyе uwezo wa kumwagilia hekta 470 ambayo ni Qash (Babati) hekta 270 na Mangisa (Mbulu) hekta 200. Skimu

saba (7) zenyenye eneo la hekta 1,551 ziliendelezwa kwenye maeneo kame chini ya Programu Shirikishi ya Kilimo cha Umwagiliaji (**Kiambatisho Na. 2**).

47. Vilevile, Wizara ilisimamia utekelezaji wa miradi 28 iliyomo katika DADPs yenye eneo la hekta 4,121 (**Kiambatisho Na. 3**) na skimu 13 zilizoendelezwa kwa kutumia fedha za Serikali na Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula zenyenye jumla ya hekta 3,650 (**Kiambatisho Na. 4**). Aidha, katika kuhamasisha matumizi bora ya maji na yenye ufanisi katika uzalishaji wa mazao, Wizara imesimamia uanzishwaji wa mashamba madogo ya mfano ya umwagiliaji kwa njia ya matone (*drip irrigation*) kwa mazao ya mboga katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwenye ukanda wa kijani wa mwambao wa Ziwa Viktoria katika wilaya za Ilemela, Nyamagana, Magu, Bukoba Vijijini, Maswa na Tarime ambapo hekta 235 ziliendelezwa (**Kiambatisho Na. 5**). Maeneo mengine ni: chuo cha wakulima cha Mkindo (Morogoro), Bihawana (Dodoma Vijijini), na Kanda za umwagiliaji za Kilimanjaro, Mwanza na Mtwara. Aidha, ujenzi wa mabanio ya skimu nne (hekta 360) kwenye ukanda wa kijani wa mwambao wa Ziwa Nyasa umekamilika. Skimu hizo ni Kimbande (100ha), Ngido (80ha), Mkalati (120ha) na Ngingama (60ha) katika wilaya ya Mbanga. Vile vile, Wizara ilitoa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa wataalam wake 35 kuhusu teknolojia mbalimbali za umwagiliaji ikiwa ni pamoja na umwagiliaji kwa njia ya matone.

48. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) imeendelea na maandalizi ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji na Mkakati wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji nchini. Sera na mkakati huo zinalenga kuonyesha dira ya utekelezaji sahihi wa maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji kwa kuzingatia sheria na kanuni zitakazohakikisha ufanisi kwa kufuata misingi ya kitaalaam na kuhakikisha

umiliki wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kulingana na mwelekeo ulioainishwa katika Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (NIMP 2002).

Uendelezaji wa Zana za Kilimo

49. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, jumla ya vituo 12 vya maksai vilikarabatiwa na kupatiwa zana timilifu ili kutoa mafunzo na kufanya maonyesho kwa wakulima. Vituo vilivyo karabatiwa ni; Sikonge FDC (Sikonge), Konje (Handeni), Inonelwa (Misungwi), Kifunda (Rungwe), Kipalapala (Tabora mjini), Malagarasi (Kigoma), Katumba Azimio (Sumbawanga), Kibakwe (Mpwapwa), Milama (Mvomero), Ngimu (Singida), Gairo (Kilosa) na Ngana (Kyela). Lengo la kukarabati vituo 25 halikufikiwa kutokana na kutokutolewa kwa fedha zote zilizoidhinishwa. Mafunzo juu ya matumizi ya zana za kilimo hifadhi yalitolewa kwa wakulima kwa mfumo wa shamba darasa na wakulima 3,675 walijifunza kwa vitendo matumizi ya zana hizo. Aidha, wizara kwa kushirikiana na wadau wa kilimo, ilitayarisha mkakati wa kuendeleza matumizi sahihi ya zana nchini. Vilevile, Wizara kwa kushirikianana na Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundii Vijijini (CARMATEC) iliyafanya majaribio ya kuhakiki ubora wa matrekta aina ya EUROPAD kutoka India na PHOTON, CATIC na KAMA kutoka China na yalionekana yanafaa kwa Tanzania.

Matumizi Bora ya Ardhi

50. Mheshimiwa Spika, ardhi ya kilimo ni raslimali muhimu katika uzalishaji wa kilimo. Raslimali hii inazidi kupoteza ubora wake kutokana na sababu mbalimbali, lakini iliyo kubwa ni kutozingatia kwa hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi. Katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo ili kuchangia katika juhudzi za

taifa za kuongeza uzalishaji wa kilimo na kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira. Kazi zilizoteklezwa ni pamoja na:

- Kukusanya maoni ya wadau wa kilimo ili yajumuishwe kwenye Mpango Kabambe wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo ambao umeanza kuandaliwa;
- Kukusanya mapendeleko ya wadau wa kilimo kwa ajili ya kuandaa muswada wa Sheria ya Kilimo ambayo itatambua, italinda na itaelekeza uendelezaji wa maeneo ya Kilimo nchini;
- Kutambua na kuhakiki maeneo yanayofaa kwa ajili ya uwekezaji katika Kilimo mikoa ya Pwani, Morogoro, Tanga na Dodoma.
- Kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani na wakulima kuhusu matumizi bora ya ardhi katika maeneo yaliyoathiriwa na mmomonyoko wa udongo, kwenye mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani, Mbeya, Singida, Kilimanjaro na Arusha.

Miradi ya Maendeleo

Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project*)

51. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea na utekelezaji wa mradi wa PADEP ambao unatekelezwa katika mikoa 10 ya Tanzania bara (Mtwara, Lindi, Morogoro, Iringa, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Tabora na Singida) na mitano ya Tanzania Visiwani (Mjini Magharibi, Kusini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba). Mradi uliwezesha utayarishaji na utekelezaji miradi mipy ya vikundi 880. Aidha, mradi ulitoa mafunzo kwa wawezeshaji katika ngazi ya kata na wilaya kutoka halmashauri 29 kwa lengo la kuwaongeza uwezo wa kuwezesha

jamii na vikundi nya wakulima kutambua matatizo yanayowakabili na kuibua miradi ya kukabiliana nayo. Wawezeshaji wamewezesha jamii na vikundi nya wakulima kutekeleza miradi 3,252 katika vijiji 552 ambayo imenufaisha kaya 490,000 kwa kupatiwa teknolojia bora. Vile vile, mradi uligharamia ukarabati wa maabara ya udongo ya UKiriguru na ununuzi wa vifaa nya maabara za udongo katika vituo nya utafiti nya UKiriguru, Uyole na Mlingano.

Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Programme Support*)

52. Mheshimiwa Spika, Programu hii inatekelezwa katika ngazi ya taifa na katika mikoa ya Iringa na Mbeya. Sehemu kubwa ya Programu hutekelezwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani katika mikoa hiyo. Katika mwaka 2006/2007, Programu iligharamia tafiti 10 zinazolenga kuboresha sera za kitaifa hususani zinazolenga masuala ya kilimo na mifugo, iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo (*District Agricultural Development Support-DADS*) katika halmashauri 15 za wilaya za mikoa ya Mbeya na Iringa. Kazi zingine zilikuwa ni kugharamia ununuzi wa vitendea kazi yakiwemo magari manane na pikipiki 100 kwa maafisa ugani wa wilaya zinazotekeliza programu. Vilevile, Programu iliwezesha wakulima wadogo kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa tani 191.7 za mazao mbalimbali. Aidha, Programu iligharamia mafunzo kwa wakulima 1,027 kutoka vijiji 480 katika halmashauri 18 katika mikoa ya Iringa, Dodoma, Mtwara, Morogoro na Lindi kuhusu uzalishaji wa mbegu za daraja la kuazimiwa.

Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agricultural Sector Investment Project*)

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agricultural Sector Investment*

Project- DASIP) unaotekelozwa katika Halmashauri za Wilaya 25 za mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga uliwezesha uibuaji na utekelezaji wa miradi 71 ya kilimo katika halmashauri zinazotekeliza mradi huo. Aidha, mradi ulitoa mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujenga uwezo wa watendaji wa halmashauri hizo. Vilevile, mradi uliendelea kuwezesha halmashauri hizo kwa kuzipatia mafunzo timu za wawezeshaji za wilaya 25 zenye wajumbe 175 na timu za kata zenye wajumbe 1,904. Mafunzo hayo yalilenga zaidi katika uibuaji na utekelezaji wa DADPs. Aidha, pikipiki 100 zilinunuliwa kwa ajili ya halmashauri za wilaya hizo.

Maendeleo ya Ushirika

54. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa ushirika iliendelea kutekeleza Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika. Programu imewezesha kuimarika kwa vyama vya ushirika kwa kukamilisha chaguzi za viongozi wa vyama vya ushirika vya msingi katika mikoa ya; Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Dar-es-salaam na Morogoro. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na warajis wasaidizi wa mikoa ilisimamia uchaguzi wa viongozi wa vyama vikuu vya ushirika vya: WETCU na ICU (Tabora); MBOCU, MICU, KYECU, RUCU na ISAYULA (Mbeya); TANECU na MAMCU (Mtwara); ILULU (Lindi); SONAMCU (Ruvuma) na CETCU - Singida. Lengo la chaguzi hizo lilikuwa ni kupata viongozi waadilifu na wenyе upeо katika masuala ya uongozi na pia kuwezesha vyama hivyo kufanya maboresho yaliyokusudiwa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali katika mkoa wa Mwanza imeweza kusimamia marekebisho katika utendaji wa chama kikuu cha Nyanza kwa kuteua wajumbe 3 kuingia kwenye bodi ya NCU. Wajumbe hao waliteuliwa kwa kutumia Sheria Na. 20, ya Vyama vya Ushirika (Cooperatives Societies Act, 2003) Kifungu Na. 127 (1) – (3). Kwa bahati mbaya wajumbe hao wote

watatu wamefariki dunia tarehe 24 Juni, 2007 wakiwa katika safari ya kikazi yenye nia ya kuimarisha ushirika. Serikali itaendelea na nia yake ya kuimarisha NCU.

55. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilifanya uhamasishaji mkubwa wa wananchi ili wajunge pamoja na kuanzisha vyama vya ushirika. Jumla ya SACCOS mpya 1,441 na vyama vya ushirika wa mazao (AMCOS) 43 vimeanzishwa nchini mwaka, 2006/2007. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa SACCOS 25 za mikoa ya Pwani, Dar-es-salaam na Arusha kuhusu modenaizesheni ya SACCOS ikiwa ni pamoja na kubadili mifumo ya uendeshaji. Vilevile, Wizara iliandaa miongozo ya Uhasibu na Menejimenti ya fedha za SACCOS na Mifumo ya Menejimenti ya Taarifa.

56. Mheshimiwa Spika, maafisa ushirika 21 wa Mikoa na 139 wa wilaya walipewa mafunzo ya uhamasishaji na uimarishaji, ukaguzi na usimamizi wa vyama vya ushirika. Aidha, walipewa mafunzo ya kuawezesha kufahamu na kutekeleza kwa ufanisi Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini.

57. Mheshimiwa Spika, Wizara ilipitia makisio ya mapato na matumizi ya vyama vya ushirika 49 pamoja na maombi ya ukomo wa madeni kwa lengo la kuviwezesha kuboresha maombi ya mikopo ili yakidhi mahitaji ya benki. Vyama vilivyokidhi mahitaji ya utayarishaji ukomo wa madeni vilipewa hati ya uthibitisho. Aidha, vyama husika vilishauriwa kuzingatia masharti ya mikopo.

Kurekebisha na Kuhuisha Sheria

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea na mchakato wa kurekebisha na kuhuisha sheria ili kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya sasa na malengo ya kutungwa kwa sheria hizo. Kazi zilizotekelzwa ni

pamoja na kuandaa rasimu ya awali ya mapendekezo ya mfumo wa kisheria unaofaa kwa ajili ya kutambua, kulinda na kuendeleza ardhi ya kilimo, kufanya mapitio ya sheria na kanuni za sekta ya kilimo na kukamilisha mchakato wa kupata maoni ya wadau mbalimbali wa mazao yanayosimamiwa na Bodi za Mazao kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sheria na kanuni za mazao hayo.

Maendeleo ya Watumishi

59. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea na zoezi la kuwapandisha watumishi vyeo kwa kuzingatia sera ya menejimenti na ajira katika utumishi wa umma pamoja na kuajiri watumishi wapya. Watumishi 972 walipandishwa vyeo na 268 kuajiriwa. Shughuli zingine zilizoteklezwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya utawala bora na ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI kwa watumishi wa Wizara.

Changamoto

60. Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2006/2007 ni pamoja na:-

- Kufanikisha utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika;
- Kuimarisha huduma za ugani;
- Upatikanaji na utumiaji wa teknolojia za kisasa;
- Upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu;
- Uimarishaji wa matumizi ya zana za kilimo;

- Maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji;
- Hifadhi na usalama wa chakula;
- Udhibiti wa visumbufu vya mimea;
- Uimarishaji wa masoko; na
- Maendeleo ya ushirika.

V. MPANGO WA MWAKA 2007/2008

61. **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika kwa mwaka 2007/2008 zimezingatia mambo matatu muhimu.

- (i) Matokeo yaliyoainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2006/2007.
- (ii) Utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa katika mpango wa kukuza uchumi, kupunguza umasikini na hivyo kuleta maisha bora kwa watanzania (hususani) wakulima.
- (iii) Utekelezaji wa ahadi za Chama cha Mapinduzi, kama zilivyoainishwa katika Ilani ya CCM.

62. **Mheshimiwa Spika**, Ilani ya CCM inakiri kuwa:- “*Kilimo ndiyo msingi wa uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika modenaizesheni ya uchumi wa Tanzania*”. Lakini, kilimo cha kisasa ni sharti muhimu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa. Hata hivyo; Kilimo chetu kina matatizo yafuatayo:-

- (i) Wakulima walio wengi hawazijui na hawazitekelezi kanuni za kilimo bora kwa mazao wanayolima, hivyo kilimo hakina tija, na mavuno yao ni kidogo.
- (ii) Wakulima wetu kwa wastani wanalima vishamba vidogo vidogo.
- (iii) Wakulima wetu wanategemea zana duni za jadi na hasa jembe la mkono.
- (iv) Upatikanaji wa mbegu bora na mbolea haujawa na mfumo wa uhakika na matumizi yake hayaenei kwa wakulima.
- (v) Karibu kazi zote za kilimo zinategemea nguvu kazi ya binadamu na hasa wanawake.
- (vi) Maji ya mvua yanaendelea kuachwa yaende baharini badala ya kuyakinga kwenye visima, malambo na mabwawa, kwa matumizi ya watu, mifugo na kilimo cha umwagiliaji maji.

63. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matatizo hayo ya kilimo, mpango wa 2007/08 utaweka mkazo katika maeneo yafuatayo:

- i) Kufanikisha utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika.
- ii) Kuimarisha huduma za ugani;
- iii) Upatikanaji na utumiaji wa teknolojia za kisasa;
- iv) Upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu;
- v) Uimarishaji wa matumizi ya zana za kilimo;

- vi) Maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji;
- vii) Hifadhi na usalama wa chakula;
- viii) Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea;
- ix) Uimarishaji wa masoko; na
- x) Maendeleo ya Ushirika.

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP)

64. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2007/2008 ni wa pili kutekeleza Programu hiyo, ambayo imetengewa shilingi bilioni 83.4. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 58.7 zimetengewa Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Wilaya DADPs. Kazi kubwa mwaka huu ni kutekeleza DADPs ambazo zimeandaliwa na Halmashauri. Kama ambavyo imesemwa mara nyingi, mafanikio katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, yatategemea ufanisi wa utendaji katika ngazi ya Wilaya. Hadi mwezi Juni, 2007 wilaya zote zilikuwa zimewasilisha mipango yao ya kilimo. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI, Wakuu wa Mikoa na Wilaya itafuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mipango ya Kilimo Wilayani ili kuhakikisha thamani ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo ya kilimo katika wilaya mbalimbali nchini inalingana na kazi zilizofanyika.

65. Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Taifa, shilingi bilioni 23.7 zimetengwa kwa Wizara za Sekta ya Kilimo kwa ajili ya kuboresha huduma za kilimo (utafiti na ugani); kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, uendelezaji wa masoko na sekta binafsi, uhakika wa upatikanaji wa chakula pamoja na uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya Programu katika ngazi ya taifa. Vilevile, kwa kutumia fedha hizo, uwezo wa Halmashauri wa

kuibua miradi na kuandaa taarifa za utekelezaji utaendelea kujengwa. Viongozi wa mikoa na Wilaya wataendelea kuhamasishwa kuhusu kuweka kipaumbele katika kusimamia na kuzijengea Halmashauri uwezo wa kufuutilia utekelezaji wa Programu na kutoa taarifa. Aidha, Sekretariati za Mikoa zitajengewa uwezo wa kufuutilia na kuratibu DADPs ili ziweze kusaidia Halmashauri wakati wa kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Hatua hii inakusudia kusogeza huduma ya usimamizi, uandaaji wa mipango mizuri ya DADPs na Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Vijijini (*Village Agricultural Development Plans -VADPs*) karibu na Halmashari na wakulima wenyewe.

Huduma za Ugani

66. Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto zinazotukabili ili kuleta mapinduzi ya kilimo, ni pamoja na kufikisha maarifa ya kilimo bora kwa wakulima. Kutokana na wakulima kutojua, na hivyo kutozingatia kanuni za kilimo bora, tija ya mazao nchini, ni ya chini sana ukilinganisha na tija inayowezekana kwa kutumia utaalam. **Tazama kiambatisho Na. 6**

67. Mheshimiwa Spika, ili tuondokane na hali hiyo na kama nilivyoeleza katika taarifa ya utekelezaji, Serikali imeamua kuchukua hatua za makusudi kuimarisha huduma za ugani, kwa nia ya kuwa na Mtaalam wa Ugani katika kila kijiji, kata na tarafa ifikapo mwaka 2010/2011, ili kufikisha maarifa na teknolojia ya kilimo kwa wakulima.

68. Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma hiyo, hatua zifuatazo zitachukuliwa:-

(i) Kuongeza Idadi ya Wataalam wa Ugani

Katika mwaka 2007/2008 wataalam wa ugani 2,500 wataajiriwa kupitia TAMISEMI na ajira itaendelea kila mwaka kwa muda wa miaka minne ambapo pengo lililopo la wataalam wa ugani 11,703 litakuwa limezibwa. Kati ya wataalam 2,500 watakaoajiriwa, wataalam 500 watakuwa wahitimu wa Chuo Kikuu ambao watatoa huduma katika ngazi ya Tarafa. Ili kuwawezesha kufanya kazi vizuri, Serikali itawaandalia mazingira mazuri kwa:-

- Kuwapatia vyombo vyta usafiri, mawasiliano na vitendea kazi kwa awamu kupitia ruzuku ya kujenga uwezo inayotolewa kwa kila halmashauri;
- Kujenga Nyumba za Kuishi kwa kushirikiana na wananchi; na
- Kujenga Vituo vyta Taaluma Katika Ngazi ya Kata (*Ward Resource Centres*) kwa kutumia ruzuku ya ushindani ya kujenga uwezo inayotolewa kwa halmashauri.

(ii) Kupanua Uwezo wa Vyuo vyta Kilimo

Ili Mpango wa Kuimarishe huduma za ugani uwe endelevu, ni muhimu kuwepo wataalam wa kilimo kwenye soko la ajira kila mwaka. Wataalam hao watatakiwa kutoka kwenye vyuo mbalimbali vyta mafunzo ya kilimo. Hivyo, tunahitaji kuongeza uwezo wa vyuo vyta kilimo wa kuchukua wanafunzi. Kazi zitakazofanyika ni;

- Kujenga na kukarabati mabweni na nyumba za wakufunzi;

- Kuajiri wakufunzi 116 wa vyuo vya kilimo kuanzia mwaka 2007/2008 hadi kufikia wakufunzi 258 ifikapo mwaka 2010/2011; na
- Kununua vifaa vya mafunzo ya kilimo;

(iii) Kutoa Mafunzo kwa Vijana Tarajali

Mafunzo yatatolewa kwa vijana 8,500 ili kuwezesha kufikia lengo la kuajiri wataalam wa ugani 11,703 ifikapo mwaka 2010/2011. Kwa kuanzia, katika mwaka 2007/2008, jumla ya vijana tarajali 3,000 watapatiwa mafunzo katika vyuo vya kilimo ili kuandaa wataalam wenyewe sifa ya kuajiriwa katika mwaka 2008/2009.

Huduma za Utafiti

69. Mheshimiwa Spika, ili kupata teknolojia sahihi zinazokidhi mahitaji ya kilimo na kuhakikisha kwamba matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima, Wizara itaendelea kufanya utafiti wa mazao kama ifuatavyo:-

- Kutathmini aina za mbegu mpya za mazao zenye tija kubwa, kustahimili ukame, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na zinazokidhi viwango vya ubora na matakwa ya walaji wa ndani na nje ya nchi;
- Kubuni na kutathmini mbinu shirikishi za udhibiti visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao;
- Kutathmini madawa asilia na ya viwandani yanayofaa kutumika nchini;
- Kusambaza matokeo ya utafiti uliofanyika;

- Kutunza na kuzalisha mbegu mama za mazao ya jamii ya nafaka, mikunde na ya mbegu za mafuta na mazao ya jamii ya mizizi;
- Kuendeleza utafiti wa mazao ya bustani kwa lengo la kupata vipando bora;
- Kutathmini viwango vyta matumizi ya mbolea vya sasa kwa lengo la kutoa mapendekezo ya viwango sahihi kulingana na hali ya udongo, hewa na aina ya zao linalozalishwa katika eneo husika;
- Kuzalisha na kusambaza miche bora ya chai 9,000,000 na kahawa miche 10,000,000 kupitia taasisi za utafiti za TRIT na TaCRI kwa wakulima na vikundi vya wakulima.

Pembejeo na Zana za Kilimo

70. Mheshimiwa Spika, pembejeo za kilimo hususan mbolea, mbegu bora na madawa ya kuua wadudu ni muhimu sana katika kuleta mapinduzi ya kilimo. Bila pembejeo hizi hakuna mapinduzi ya kilimo. Kwa kuzingatia umuhimu huo wa pembejeo, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea, mbegu bora na madawa ya mimea. Jumla ya shilingi 19.5 bilioni zimetengwa kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo. Kama nilivyoainisha katika taarifa ya utekelezaji, bado mfumo wetu wa kufikisha pembejeo zenye ruzuku kwa wakulima, unakabiliwa na matatizo.

Pamoja na jitihada iliyochukuliwa ya kusimamia usambazaji wa mbolea na kuifikisha katika vituo 24 katika mikoa yote nchini, bado umejitokeza upungufu katika mfumo wa usambazaji hasa katika kufikisha mbolea na mbegu kwa wakulima na kwa wakati. Upungufu uliojitokeza ni pamoja na;

- i) Mbolea kutofika wilayani, kwa wakati kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa mawakala ;
- ii) Vituo vikuu vya kununulia mbolea mkoani kuwa mbali na wakulima;
- iii) Kuwepo kwa bei mbili za mbolea katika soko moja, yaani bei ya mbolea yenyeye ruzuku na bei ya mbolea isiyo na ruzuku, kutokana na ufinyu wa bajeti; na
- iv) Kutokuwepo kwa takwimu sahihi za mahitaji halisi ya pembejeo.

71. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2007/2008, Wizara itaendelea kuchukua hatua za kuboresha utaratibu wa ruzuku unaotumika hivi sasa kwa kutoa ruzuku kulingana na mahitaji ya aina ya pembejeo na mazao katika kanda zote nchini kama ifuatavyo:

- (a) Ingawa tulipeleka mbolea katika kila mkoa nchini, na ingawa ni kweli mbolea inahitajika katika mikoa yote, ni dhahiri kwamba iko mikoa inayotumia mbolea zaidi hasa kwa zao la mahindi ambalo linatoa mchango mkubwa kwa usalama wa chakula kwa Taifa. Kwa msingi huo, katika mwaka 2007/2008, sehemu kubwa ya mbolea itaelekezwa katika mikoa inayozalisha mahindi kwa wingi. Ili kupunguza tatizo la umbali kutoka Makao Makuu ya Mikoa, tutaongeza vituo vya usambazaji wa mbolea, hasa katika mikoa inayotumia mbolea kwa wingi.
- (b) Ruzuku kwa ajili ya madawa ya kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu itatolewa kwa mazao ya Pamba na Korosho: madawa ya pamba lita 1,200,000 na madawa ya

korosho lita 50,000 za madawa ya maji na tani 1,100 za madawa ya unga; na

- (c) Ruzuku kwa ajili ya miche bora 5,000,000 ya kahawa na 5,000,000 ya chai, yenye tija kubwa, inayokomaa mapema na yenye ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vyat mazao hayo itatolewa.

MAANDALIZI KWA AJILI YA MAPINDUZI YA KIJANI (GREEN REVOLUTION)

72. Mheshimiwa Spika, kama nilivyolifahamisha Bunge letu Tukufu mwaka jana, juu ya Tamko la Abuja la Mapinduzi ya Kijani ya Afrika (*Abuja Declaration on the Africa Green Revolution*) nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo :

Tumefikia makubaliano na *Rockefeller Foundation* na *Bill and Melinda Gates Foundation*, Mashirika mawili yanayoshirikiana na mashirika mengine mengi duniani katika kuunga mkono juhudzi za mapinduzi ya kijani katika Afrika, kuanza maandalizi katika mwaka 2007/2008 kwa kufanya yafuatayo:

- Kuandaa mawakala wa pembejeo za kilimo vijijini (*rural agro-dealers*) kwa kuwapa mafunzo na kuwawezesha kupata mikopo ili kupitia kwao, pembejeo ziweze kuwafikia wakulima.
- Kusaidia uzalishaji wa mbegu za aina mbalimbali (*seed multiplication*) ili ziwepo mbegu za kutosha kwa ajili ya wakulima;
- Kuyawezesha makampuni kusambaza mbolea, mbegu na madawa hadi vijijini kulingana na mahitaji ya pembejeo hizo hapa nchini;

- Kuandaa vocha ambazo haziwezi kugushiwa. Kupitia mfumo huo wa vocha (hati punguzo), ruzuku itatolewa moja kwa moja kwa mkulima badala ya kutoa ruzuku kwa makampuni yanayoagiza/kusambaza mbolea au makampuni ya uchukuzi.

73. Mheshimiwa Spika, uongozi wa Shirika la *Rockfeller Foundation* na *Bill & Melinda Gates Foundation*, umekubali mpango uanze Tanzania, kwa sababu, kuna uongozi unaokerwa na umasikini na una mkakati wa kupambana na umasikini (MKUKUTA). Aidha, kwa maneno yao wenyewe, kuna “*political will*”, na kuna Rais ambaye anajali.

74. Mheshimiwa Spika, Mpango huo ukifanikiwa, kuanzia mwaka 2008/2009, pembejeo zitakuwa zinapatikana vijijini wakati wowote kama soda ya Coca cola inavyopatikana popote. Tukifikia hatua hiyo, na kwa mtandao wa wataalamu wa ugani, watakaokuwepo kila kijiji na kata, mapinduzi ya kijani (*Green Revolution*) yatakuwa yameshika kasi mpya na nguvu mpya.

Mfuko wa Pembejeo

75. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo kwa mwaka 2007/2008, umetengewa jumla ya shilingi bilioni 3.5 na utaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana bora za kilimo kupitia benki mbalimbali na Shirikisho la vyama vyta Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT). Mikopo itatolewa kwa mbolea , madawa ya mimea na ya mifugo, majembe ya kukokotwa na wanyama kazi, matrekta madogo aina ya *power tiller* 50, matrekta makubwa mapya 100 na kukarabati matrekta mabovu 12. Aidha, Mfuko utaendelea kuboresha utaratibu wa kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo ili kuhakikisha wakulima wanapata huduma kwa wakati unaofaa na kwa bei nafuu. Mfuko

pia utaendelea kukusanya madeni ya miaka ya nyuma ili kutoa mikopo kwa wakopaji wengi zaidi.

Zana za Kilimo

76. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundsi Vijijini (CAMARTEC) itafanya tathmini katika kila kanda ili kutambua mahitaji ya aina ya zana zinazofaa kutumika katika kanda hizo. Aidha, Wizara itaandaa mwongozo wa teknolojia mbalimbali za zana za kilimo ambazo zinaweza kutumika nchini kulingana na hali ya udongo. Vilevile, wataalamu 70 wa zana watapewa mafunzo ya matumizi bora ya zana za kilimo zikiwemo zana za kilimo hifadhi na zana za usindikaji wa mazao.

Hifadhi ya Udongo na Matumizi Bora ya Ardhi

77. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itasisitiza matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na kuhakikisha ushiriki wa wakulima katika kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi endelevu ya ardhi kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji na kuhifadhi mazingira. Aidha, Wizara itaendelea na maandalizi ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi ambao utakuwa ni msingi wa uandaaji wa mipango, matumizi na usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kilimo. Kazi nyingine zitahusu kuhakiki na kutambua maeneo yanayofaa kwa uwekezaji katika kilimo na kupima maeneo ya umwagiliaji. Vilevile, Wizara itandaa mapendekezo kwa ajili ya kutunga sheria itakayotumika kutambua na kulinda ardhi ya kilimo.

Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani

78. Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, Wizara imepanga kuendeleza jumla ya hekta 153,188 katika hatua za ujenzi (hekta 21,035) na upembuzi yakinifu na usanifu (132,153) katika sehemu mbalimbali. Kati ya hizo, hekta 16,150 ni skimu za umwagiliaji wa asili za wakulima wadogo ambazo zitafanyiwa ukarabati (**Kiambatisho Na. 7**). Aidha, ujenzi wa mabwawa madogo 16 katika maeneo ya mikoa ya Manyara, Tabora, Mwanza, Singida, Dodoma, Iringa, Mara, Shinyanga na Tanga utatekelezwa kwa kulenga kumwagilia hekta 4,085 (**Kiambatisho Na. 8**). Mabwawa 9 yenye uwezo wa kumwagilia eneo la hekta 10,150 yatafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika wilaya za Mbarali, Kyela, Magu, Nzega na Kibondo kama ilivyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na. 9**. Vile vile skimu 85 za umwagiliaji zenyenye eneo la hekta 78,950 zitafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali katika kanda zote saba za umwagiliaji kama ilivyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na. 10**.

79. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/08, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuendeleza teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika maeneo yanayozunguka ziwa Viktoria, ziwa Nyasa na maeneo mengine nchini. Aidha, uhamasishaji na usimamizi katika matumizi ya teknolojia za kutumia pampu za kusukuma maji kwa miguu, upepo, mionzi ya juu na dizeli utatekelezwa.

80. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza umwagiliaji kwenye miradi ya ukubwa wa kati, Wizara itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa mradi wa Madibira awamu ya pili (hekta 3,600), ambao utapata maji ya umwagiliaji kutoka katika bwawa litakalojengwa na Wizara ya Maji katika mto Ndembera.

81. Mheshimiwa Spika, ili kuitikia agizo la Mheshimiwa Rais la kuendeleza kilimo cha Umwagiliaji na kuufanya mkoa wa Morogoro uwe ghala la Taifa la nafaka, Wizara itaendelea kutekeleza ujenzi wa skimu mbili (2) za umwagiliaji za Minepa hekta 600 (Ulanga) na Wami-Luhindo hekta 200 (Mvomero). Aidha, jumla ya skimu 37 zenyenye eneo la hekta 32,879 zitafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika wilaya za Morogoro vijijini, Kilosa, Ulanga, Kilombero na Mvomero kama ilivyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na. 11.** Vile vile, miradi ya umwagiliaji iliyoinishwa katika DADPs iteteklezwa kwa ushirikiano na Halmashauri.

82. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/08 Wizara itaendelea na maandalizi ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji na Mkakati wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji nchini.

Usalama wa Chakula

83. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo wataalam wa kilimo wa halmashauri za wilaya kwa kuwapatia mafunzo ya teknolojia mbalimbali za usindikaji wa mazao ya chakula, hususan yale ya nafaka, mikunde, muhogo, mboga na matunda. Aidha, mafunzo ya utayarishaji wa mazao ya mtama, muhogo, mboga na matunda yatatolewa kwa lengo la kupanua matumizi ya mazao hayo ili kuongeza uhakika wa chakula. Kama sehemu ya kupanua soko la zao la muhogo, Wizara itawahamasisha wasindikaji wakubwa wa mazao ya nafaka kuchanganya unga wa muhogo na unga wa nafaka kama vile mahindi na mtama kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo.

84. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri kuibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula katika ngazi ya kaya kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Mafunzo hayo yatahusu teknolojia za kukadiria maeneo yaliyolimwa mazao (*Geographical Information System – GIS* na *Geographical Positioning System -GPS*), ukusanyaji wa takwimu na taarifa za mvua na hali ya mazao mashambani na teknolojia za usindikaji na hifadhi ya mazao.

85. Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani yanayosababisha athari katika maeneo mbalimbali, Wizara itafanya tafiti kwa lengo la kubaini sababu za baadhi ya maeneo, hususan katika mikoa ya kati kuwa na upungufu wa mara kwa mara wa chakula. Lengo la tafiti hizo ni kuandaa mikakati ya kupata ufumbuzi wa kudumu wa kukabiliana na hali hiyo. Ili kuiwezesha Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na upungufu wa chakula, Wizara itaendelea kufanya savei za utabiri wa uzalishaji wa mazao ya chakula ili kubaini hali ya chakula nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini za kina katika maeneo yatakayobainika kuwa na upungufu wa chakula ili kutambua kaya zenye upungufu na hatua za kuchukuliwa.

Akiba ya Taifa ya Chakula

86. Mheshimiwa Spika, Akiba ya Taifa ya Chakula imepanga kununua tani 27,500 za mazao ya nafaka, vitendea kazi na madawa ya kuhifadhi nafaka. Kazi zingine zitakazofanyika ni pamoja na kuhamisha chakula kutoka kanda zenye ziada ya chakula na kukipeleka kwenye kanda zitakazokuwa na upungufu. Aidha, Akiba ya Taifa ya Chakula itaanza kuendesha shughuli zake kwa mfumo wa Wakala wa Serikali.

Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea

87. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2007/2008, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuimarisha huduma ya utabiri wa milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mazao kwa lengo la kudhibiti uharibifu kabla ya kushambuliwa kwa mazao. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kutumia udhibiti husishi wa visumbufu vya mimea na mazao katika mikoa ya Kigoma, Singida, Mtwara, Lindi, Morogoro, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Kagera, Mwanza na Mara ambako milipuko ya visumbufu hutokea mara kwa mara. Wizara pia itaendelea na udhibiti wa gugumaji, ugonjwa wa mnyauko wa migomba (*banana bacterial wilt*), batobato kali ya muhogo na mashambulizi ya nzi wa matunda kwenye maeneo yanayozalisha mazao hayo kwa wingi.

Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara

88. Ili kuhakikisha kwamba tija, uzalishaji na ubora wa mazao ya biashara vinaongezeka, Wizara kupitia Bodi za Mazao itaendelea kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uzalishaji wa mazao makuu ya biashara kama ifuatavyo:-

Kahawa

89. **Mheshimiwa Spika**, uzalishaji kahawa msimu 2007/2008 unatarajiwा kuwa tani 52,000. Mikakati ya kufikia kiwango hicho ni pamoja na kuongeza kasi ya upandaji miche bora yenye ukinzani dhidi ya magonjwa, kuboresha huduma za ugani, kuhimiza kilimo cha umwagiliaji maji katika maeneo yanayozalisha kahawa na kuhamasisha soko la ndani la unywaji wa kahawa, kuwahimiza wakulima kuongeza matumizi ya zana bora za kumenya kahawa ili kuongeza ubora.

Chai

90. **Mheshimiwa Spika**, matarajio ya uzalishaji wa chai msimu wa 2007/2008 ni tani 36,000. Mikakati ya kufikia lengo hilo ni pamoja na

kuhamasisha matumizi ya vipando bora na kuimarisha huduma za ugani. Mikakati hiyo ina lengo la kuongeza tija kutoka wastani wa kilo 1,900 kwa hekta hadi kilo 2,350 kwa hekta kwa wakulima wakubwa na kutoka kilo 850 kwa hekta hadi 950 kwa hekta kwa wakulima wadogo.

Korosho

91. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2007/2008, uzalishaji wa korosho unatarajiwa kuwa tani 141,000. Mkazo utawekwa katika kuendeleza na kuboresha kilimo cha korosho kwa kufuata kanuni za kilimo bora, kudhibiti wadudu na magonjwa ya korosho kwa kutoa ruzuku kwenye viuatilifu, kuimarisha huduma za ugani na kuhamasisha uwekezaji katika ubanguaji wa korosho ili kuongeza thamani ya zao hilo na kutoa ajira.

Pamba

92. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa pamba nyuzi katika msimu wa 2007/2008 unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 130,565 za msimu 2006/2007 hadi tani 300,000, sawa na ongezeko la asilimia 130. Lengo lilikuwa ni kuzalisha tani 410,000. Hata hivyo, lengo hilo halitafikiwa kutokana na mvua kuzidi wakati wa kupanda. Katika maeneo ya tambarare, maji yalituama na kuozesha mbegu zilizokuwa zimepandwa, maji yalidumaza pamba iliyokuwa imeota na pia maji yalichelewesha upandaji katika maeneo mengine. Mikakati ya kuongeza uzalishaji wa pamba ni pamoja na kuhakikisha madawa yenyeye ruzuku na mabomba ya kupulizia yanawafika wakulima kwa wakati.

Tumbaku

93. Mheshimiwa spika, uzalishaji wa tumbaku msimu wa 2007/2008 unatarajiwa kuwa tani 80,000. Ili kufikia uzalishaji huo, mbolea yenyeye ruzuku itafikishwa kwa wakulima kwa wakati. Wakulima wapya 7,000 na wazalishaji wawili wa mbegu bora za tumbaku watasajiliwa, mashamba, vituo vya kuuzia

tumbaku, na viwanda vya tumbaku vitakaguliwa ili kuhakikisha sheria na kanuni za tumbaku zinazingatiwa.

Sukari

94. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa sukari katika msimu wa 2007/2008 unatarajiwa kuwa tani 312,000. Ili kufikia lengo hilo, Wizara kupitia Bodi ya Sukari itaendelea na usimamizi na uratibu wa shughuli mbalimbali zinazolenga kuongeza tija na uzalishaji wa sukari. Mkazo utawekwa katika utafiti wa mbegu mpya za miwa zilizotoka Afrika ya Kusini, Mauritius na Reunion ili kupata mbegu bora, kutoa mafunzo ya kilimo bora cha miwa, hususan udhibiti wa wadudu na magonjwa, kuwakutanisha wazalishaji na wanunuzi katika kujadili bei ya miwa, kuhamasisha wakulima wadogo wa sukari kuongeza uzalishaji na wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika sekta ya sukari nchini.

Pareto

95. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2007/2008, uzalishaji wa pareto unatarajiwa kuwa tani 2,200. Uzalishaji huo utatokana na kuongeza eneo linalolima pareto toka hekta 6,000 msimu 2006/2007 hadi hekta 10,000 msimu 2007/2008. Ili kufikia lengo hilo, kazi zitakazofanyika ni kusambaza tani 20 za mbegu bora na kugharamia *bulking centers* sita za kuzalisha vikonyo vya miche kuinua tija ya pareto toka kilo 400 msimu 2006/2007 hadi kilo 500 kwa hekta. Aidha, wakulima watahamasishwa kujiunga na vyama vya wakulima wa pareto ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za uzalishaji wa pareto.

Mkonge

96. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mkonge katika msimu 2007/2008 unatarajiwa kuwa tani 46,000. Ili kufikia lengo hilo, mikakati itakayotumika ni pamoja na kutumia njia bora za kilimo, kufufua mashamba ya zamani,

kuendeleza uzalishaji wa mkonge katika maeneo mapya. Mikakati mingine ni kuongeza matumizi mengine ya mkonge kwa kuzalisha umeme, chakula cha mifugo, mbolea, kutengeneza karatasi, madawa, bio-ethanol, kemikali za viwandani na vitambaa vyaa barabara (geo-textiles).

Malengo ya uzalishaji wa mazao makuu ya biashara yameonyeshwa katika **Kiambatisho Na. 12.**

Uzalishaji wa mazao ya chakula na Mbegu za Mafuta

97. Mheshimiwa Spika, ili taifa liweze kujitosheleza kwa chakula, katika mwaka 2007/2008 Wizara itaweka mkazo katika uzalishaji wa mazao makuu ya chakula, hususan mahindi, mpunga, mtama na mhogo. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itaendelea kushirikiana na halmashauri kuwahimiza wakulima kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao kuongeza eneo la uzalishaji na tija ili kufikia kiwango cha juu kinachoweza kufikiwa kulingana na hali ya udongo na kanda za mazao. Juhudi hizi zitaenda sambamba na utaratibu wa serikali wa kutoa ruzuku ya tani 84,131 za mbolea na tani 3,000 za mbegu bora za mahindi na mtama katika mikoa inayolima mazao hayo kwa wingi. Aidha, halmashauri za wilaya zitahimizwa kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) inayozingatia usalama wa chakula. Vile vile, Wizara itaendelea kushirikiana na halmashauri na sekta binafsi katika kuendeleza uzalishaji na usindikaji wa mbegu za mafuta. Mbegu hizo ni pamoja na karanga, ufuta, alizeti, kartamu, soya, michikichi na jatrofa katika mikoa yote yenyе sifa na uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao hayo.

Uendelezaji wa Mboga Matunda na Mazao Mapya

98. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, mkazo utawekwa katika kuendeleza mazao mapya ili kuongeza mchango wa sekta katika pato la taifa na ukuaji wa uchumi. Mazao yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na

mazao ya matunda, viungo, mboga, maua na mimea inayotumika kutengenezea madawa. Aidha, bustani za serikali zitaendelea kuimarishwa ili zitunze nasaba na kuzalisha vipando bora vya mazao hayo.

Uendelezaji wa mazao ya nishati na ya ukame

99. Mheshimiwa Spika, Wizara pia itaendelea kuhamasisha wadau wa mazao ya mbegu za mafuta kwa ajili ya nishati mbadala kama vile jatrofa na michikichi kwa ajili ya *bio-diesel* na miwa kwa ajili ya *bio-ethanol* kuwekeza katika uzalishaji na usindikaji wa mazao hayo. Aidha, ili kuhakikisha kuwa mazao ya nishati mbadala yanazalishwa kwa utaratibu unaoelewaka, Wizara kupitia kikundi kazi kilichoundwa na serikali itashiriki katika maandalizi ya sera juu ya uzalishaji na matumizi ya mazao ya nishati mbadala. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Magereza itaendelea kuzalisha kwa wingi zaidi vipando bora vya muhogo ili kukabiliana na kasi ya magonjwa yanayoshambulia zao hilo muhimu kwa chakula.

Kilimo cha mkataba

100. Mheshimiwa Spika, Kilimo cha mkataba kimeanza kupanuka lakini hadi sasa hakuna utaratibu maalumu na sheria inayosimamia utekelezaji wake. Wizara kwa kushirikiana na wadau inatayarisha taratibu hizo ili kuhakikisha haki za wakulima zinalindwa na pia kuepusha migogoro inayoweza kutokea.

Miradi ya Maendeleo

Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agriculture Sector Investment Project- DASIP*)

101. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara kupitia Mradi wa DASIP imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

- Kuzijengea uwezo wa kupanga na kutekeleza Mipango ya Kuendeleza Kilimo ya Wilaya (DADPs) kwa Halmashauri 25 za mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Shinyanga na Kigoma zinazotekeliza Mradi.
- Kutoa mafunzo mbalimbali kwa wakulima yatakayowawezesha kuendesha Kilimo bora cha mazao wanayozalisha na ufugaji bora.
- Kutoa mafunzo yanayohusu Uimarishaji wa vyama vyaa Kuweka na Kukopa pamoja na utafutaji wa Masoko kwa mazao wanayozalisha.
- Kununua baiskeli 500 kwa ajili ya wataalam wa kata na vijiji.

Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project*)

102. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, mradi utaendelea kutekelezwa katika wilaya 29 kutoka mikoa kumi ya Tanzania bara na mikoa mitano ya Tanzania Visiwani. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- Kuimarisha uwezo wa Wizara kutoa misaada ya kiufundi na kutekeleza shughuli za maendeleleo ya kilimo katika halmashauri za wilaya 126;
- Kuendelea kuwezesha utekelezaji wa miradi ya jamii na vikundi na programu za kuimarisha uwezo wa wilaya katika kusimamia shughuli za maendeleo ya kilimo na ushirika;
- Kuwezesha jamii kubuni na kutekeleza miradi 3,155 kwa kutumia mbinu shirikishi;
- Kuendelea kuchangia katika kuhuishwa na kurekebisha sera na kanuni mbalimbali kwa lengo la kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika masoko ya pembejeo na mazao na utekelezaji wa mradi kwa ujumla;

- Kuendelea kuwezesha taasisi za utafiti, zikiwemo maabara za udongo na vyanzo vingine vya teknolojia kupeleka teknolojia mpya kwa walengwa ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya Kilimo na mifugo;
- Kutoa mafunzo kwa wavezeshaji ngazi ya wilaya na taifa ili kuwaongezea maarifa na tija katika kuwezesha jamii na vikundi vya wakulima;
- Kugharamia vyombo vya usafiri kwa halmashauri ambazo hazina vyombo hivyo vya usafiri; na
- Kuimarisha uwezo wa sekta binafsi kushiriki na kutoa huduma zinazohitajika katika kilimo.

Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Programme Support – ASPS*)

103. Mheshimiwa Spika, Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo itaendelea kusaidia utekelezaji wa DADPs katika mikoa ya Mbeya na Iringa. Aidha, kupitia Programu hiyo, itafanya tafiti za kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Vilevile, itatoa mafunzo kwa wataalamu wa kilimo wa wilaya 18 juu ya uzalishaji mbegu za daraja la kuazimiwa (*Quality Declared Seeds*) na mafunzo ya ukaguzi wa mbegu za daraja la kuazimiwa kwa mikoa yote ya Tanzania Bara. Kazi zingine zitahusu uimarishaji wa sekta binafsi na kuhuishwa sera na sheria zinazohusu kilimo.

Uratibu wa Utekelezaji wa Sera na Sheria za Kilimo

104. Mheshimiwa Spika, Mwaka wa 2007/2008, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997, maandalizi ya mfumo wa kufuatilia na kutathmini utekeleaji wa ASDP, Sheria ya Kilimo itakayotambua, kulinda na kuendeleza maeneo ya Kilimo nchini. Aidha, Wizara itaandaa mapendekezo ya maeneo ya kuzingatiwa katika muswada wa Sheria ya Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula. Kazi nyingine zitahusu,

kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya sheria za mazao na sheria za Hifadhi ya Mimea (*Plant Protection Act*), Sheria ya Taasisi ya Viuutilifu (TPRI).

Maendeleo ya Ushirika

105. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara kupitia Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika itazingatia maeneo makuu yafuatayo:

- Kuwawezesha Maafisa Ushirika walioko Mikoani na Serikali za Mitaa kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi ili waweze kutekeleza vizuri majukumu yao;
- Kuandaa na kusambaza miongozo ya kuelekeza namna ya kuendesha Vyama vya Ushirika kibiashara kwa kuzingatia sheria na taratibu za Vyama vya Ushirika;
- Kuhamasisha wananchi kujiunga na kuanzisha Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi;
- Kukagua vyama vya ushirika kama inavyoelekeza sheria ya vyama vya ushirika; na
- Itaimarisha ushirika wa mazao ya pamba na korosho, ili kuwezesha vyama vya mazao hayo kushiriki katika ununuzi wa mazao hayo, ili kulinda bei ya mkulima.

Maendeleo ya Watumishi

106. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara itafanya yafuatayo:-

- Kuwapandisha vyeo watumishi 108 katika madaraja mbalimbali kwa kuzingatia sera ya menejimenti na ajira katika utumishi wa umma;

- Kuajiri watumishi 525 ili kuongeza nguvu kazi katika utoaji wa huduma. Kati ya watumishi hao watakaoajiriwa, watumishi 116 watakuwa wakufunzi wa vyuo vya kilimo wanaotegemewa kuongeza uwezo wa kufundisha wanafunzi tarajali 3,000 wa ugani ili kuweza kutekeleza mpango wa kuboresha huduma za ugani;
- Kuendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu mbalimbali za kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI;
- Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Rushwa pamoja na Mpango Mahsusni Kisekta (NACSAP) wa 2006-2010 na kuhimiza watumishi kuzingatia maadili ya utumishi katika utoaji huduma kwa umma;
- Kutoa mafunzo kwa watumishi 200 kuhusu namna ya kuzingatia sera ya jinsia katika upangaji na utekelezaji wa shughuli mbali mbali za kilimo;
- Kupitia na kutangaza Mkataba wa huduma kwa wateja.

VI. SHUKRANI

107. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru tena, Waheshimiwa Wabunge, hususan Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi inayoongozwa na Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje. Kamati hiyo, ilichambua kwa kina makadirio ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika na kutoa mapendekezo yatakayochangia kuboresha utekelezaji wa shughuli za kilimo nchini kwa mwaka 2007/2008. Ni matengemeo yangu kuwa, kwa nia hiyo hiyo, Waheshimiwa Wabunge watatoa maoni yao ambayo yatachangia katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

108. Mheshimiwa Spika, napenda kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yanaendelea kusaida Serikali yetu katika juhudzi za kuleta mageuzi katika Sekta ya Kilimo. Napenda kuzishukuru nchi za; Canada, China, Denmark, Finland, India, Indonesia, Ireland, Israeli, Japan, Korea Kusini, Misri na Ubelgiji. Aidha, nayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo; Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, UNDP, FAO, EU, CFC, SADC, WFP, IFAD, CIMMYT, ICRAF, ICRISAT, ASARECA, IITA, UNCTAD, JICA, UNEP na *Rockefeller Foundation* na *Bill & Melinda Gates Foundation*.

109. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa wakulima wa Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu ya ukosefu wa pembejeo muhimu, teknolojia duni na kilimo cha kutegemea mvua. Aidha, napenda kuwashukuru Wadau wote wa Sekta ya Kilimo kwa michango yao ambayo imeiwezesha Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kutekeleza mambo mengi kwa ufanisi mkubwa. Pia napenda kuwashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza (Mb), Mheshimiwa David Mathayo David (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Peniel M. Lyimo, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Mohamed Muya, Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika na taasisi zote kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii.

VII. HITIMISHO

110. Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo inatekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2005 na Sera ya Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi ili washiriki kikamilifu katika kuainisha matatizo yanayowakabili, kupanga mipango ya kukabiliana nayo, kushiriki

katika utekelezaji wa mipango hiyo na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo. Serikali itajitahidi kuweka mazingira yatakayosaidia maendeleo ya kilimo, ikiwa ni pamoja na kuongeza wataalam wa kilimo, kuboresha miundo mbinu, hususan ya umwagiliaji, maghala na barabara pamoja na upatikanaji wa pembejeo. Ni matumaini yangu kuwa kwa kuzingatia kuwa matatizo ya sekta ya kilimo ni ya mtambuka, wote tutashirikiana katika kuyapatia ufumbuzi.

VII. MAOMBI YA FEDHA ZA KWA MWAKA 2007/2008

111. Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 131,912,102,600 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Kati ya fedha hizo, shilingi 71,850,190,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 60,061,912,600 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 6,756,000,000, sawa na asilimia 11.25 ni fedha za ndani na shilingi 53,305,912,600, sawa na asilimia 88.75 ni fedha za nje.

112. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja.

Kiambatisho Na.1

**SKIMU 62 ZA UMWAGILIAJI ZILIZOFANYIWA
UPEMBUZI YAKINIFU WA AWALI NA KUSANIFIWA
MWAKA WA 2006/2007**

S/NA	JINA LA SKIMU	WILAYA	ENEO (ha)
1	Mpanga Ngalimila	Kilombero	31,500
2	Kisegese	Kilombero	7,298
3	Mguwe	Kilombero	2,270
4	Chita	Kilombero	11,650
5	Mgonya	Kilombero	9,400
6	Udagaji	Kilombero	1,700
7	Sululu	Kilombero	210
8	Kilama	Kilombero	210
9	Kiberege	Kilombero	200
10	Mgongola	Kilosa	620
11	Kiroka	Morogoro (V)	300
12	Mlilingwa	Morogoro (V)	200
13	Kongwa	Morogoro (V)	5,000
14	Tulo	Morogoro (V)	150
15	Kigugu	Mvomero	800
16	Dihombo	Mvomero	731
17	Lapiro	Ulanga	400
18	Usangule	Ulanga	1,500
19	Minepa	Ulanga	600
20	Misegese	Ulanga	1,000
21	Lapiro	Ulanga	700
22	Euga	Ulanga	440
23	Usangule	Ulanga	1,500

24	Ruaha	Ulanga	750
25	Mto wa Mbu Systems	Monduli	3,032
26	Kisese	Kondoa	2,000
27	Mikocheni	Moshi Rural	1,200
28	Kisiwani	Same	1,000
29	Mpendaroho	Hai	2,500
30	Gonja	Same	1,200
31	Pawaga	Iringa (V)	2,000
32	Mwajiginga 'B'	Kishapu	300
33	Ngeme	Kishapu	500
34	Nyenze	Kishapu	450
35	Magu	Kishapu	250
36	Kijongo	Kishapu	400
37	Ikangu-Liambasi	Bariadi	350
38	Rungwe Mpya	Kasulu	500
39	Majengo	Igunga	500
40	Igurubi	Igunga	334
41	Hanga Ngadinda	Songea	299
42	Mpitimbi B	Songea	250
43	Chiulu/Lilambo	Mbinga	400
44	Masepe/Mahimbasi	Mbinga	400
45	Msanjesi	Namtunbo	120
46	Mkwaya	Lindi	300
47	Makangaga	Kilwa	150
48	Madaba	Tunduru	150
49	Makondeko	Newala	5,000
50	Chipole	Songea	400
51	Nakahuga (dam)	Songea	400
52	Muhukuru	Songea	522
53	Nkowe	Ruangwa	450
54	Kimbande	Mbinga	750
55	Ngindo	Mbinga	320
56	Mkalati	Mbinga	642
57	Segeni	Rufiji	1,100
58	Lower Mkomazi	Korogwe	1,477
59	Chitete-Ikumbilo	Ileje	250
60	Kolandoto/Ibadakuli	Shinyanga vijijini	400
61	Makanya	Same	600
62	Kisangwa	Bunda	650
JUMLA			110,675

Kiambatisho Na. 2

SKIMU 7 ZILIZOTEKELEZWA CHINI YA PROGRAMU SHIRIKISHI YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI.

NA	JINA LA SKIMU	WILAYA	ENEO (Ha)
1.	Buhekela/Miswaki	Igunga	360
2.	Kimiza	Kwimba	175
3.	Ilujamate	Misungwi	250
4.	Mangisa	Mbulu	200
5.	Nyashidala	Misungwi	320
6.	Iyuhwa	Mpwapwa	45
7.	Msagali	Mpwapwa	201
JUMLA			1,551

Kiambatisho Na. 3

SKIMU 28 ZILIZOTEKELEZWA CHINI YA MIPANGO YA MAENDELEO YA KILIMO YA WILAYA (DADPS)

NA	JINA LA SKIMU	WILAYA	ENEO (Ha)
1.	Ifumbo	Chunya	300
2.	Kwamgumi	Korogwe	170

3.	Ilesa	Mbeya (V)	100
4.	Izumbwe	Mbeya (V)	200
5.	Mshewe	Mbeya (V)	250
6.	Mwashona	Mbeya (V)	60
7.	Ngana	Mbeya (V)	300
8.	Mfumbi	Kyela	100
9.	Mapogoro	Makete	100
10.	Iyendwe	Ileje	250
11.	Mkombozi	Mbozi	100
12.	Ipunga	Mbozi	60
13.	Orkungwado	Mbozi	80
14.	Kisamaka	Arumeru	120
15.	Maksoro Ateri	Arumeru	60
16.	Singisi	Arumeru	40
17.	Migombani Kati	Arumeru	90
18.	Kirurumo	Monduli	50
19.	Ntele	Monduli	85
20.	Makaro	Hai	128
21.	Lawate	Hai	270
22.	Mbagai – Fune	Lushoto	105
23.	Malindi, Tae, Mtii	Same	40
24.	Nyendera	Kibondo	160
25.	Tsamasi	Babati	35
26.	Endasak Basin	Hanang	168
27.	Mang'onyi	Singida Vijijini	400
28.	Kisasida	Singida MC	300
JUMLA			4,121

Kiambatisho Na. 4

SKIMU 11 ZILIZOTEKELEZWA KWA KUTUMIA FEDHA ZA SERIKALI NAMFUZO WA FACF

NA	JINA LA SKIMU	WILAYA	ENEOD (Ha)
1.	Uraroni	Rombo	1250
2.	Lundo	Mbinga	400

3.	Kitere	Mtwara	240
4.	Mbebe	Ileje	400
5.	Ngarenanyuki	Monduli	440
6.	Makangaga	Lindi	100
7.	Msanjesi	Namtumbo	120
8.	Mwiruzi	Kibondo	100
9.	Mang'ola	Karatu	200
10.	Gichameda	Babati	200
11.	Ilunda	Iramba	200
JUMLA			3,650

Kiambatisho 5

MAEneo YALIYOENDELEZWA KATIKA UKANDA WA KIJANI WA MWAMBAO WA ZIWA VIKTORIA

NA	WILAYA	Idadi ya Vikundi	ENEo (Ha)
1.	Ilemela	28	56
2.	Nyamagana	33	66
3.	Magu	25	12
4.	Bukoba Vijijini	16	16
5.	Maswa	30	25
6.	Tarime	30	60
JUMLA			235

Kiambatisho Na. 6

MAZAO YA CHAKULA

Na.	Zao	Upatikanaji wa Maji	Tija ilivyo hivi sasa (kg/ha)	Tija inavyowezekana (kg/ha)
1.	Mahindi	Kwenye maeneo yenye Mvua za wastani	600 – 2,200	5,000
		Katika yenye mvua nyingi	1,000 – 3,000	7,500
2.	Mpunga	Kwa kutegemea kilimo cha mvua	2,900	4,000 – 4,500
		Kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani	3,500 – 4,500	6,000
3.	Mtama na		640	3,500

	Uwele		
--	-------	--	--

MAZAO YA BIASHARA

Na.	Zao	Tija ilivyo hivi sasa (kg/ha)	Tija inavyowezekana (kg/ha)
1.	Kahawa	100 – 170	2,000
2.	Pamba:		
	Kanda ya Mashariki	500	3,000
3.	Kanda ya Magharibi	500	3,500
	Tumbaku (ya mvuke)	950 – 1,000	1,800
4.	Tumbaku Moshi	950	1,800
	Chai	400	2,000

Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula

Kiambatisho Na.7

SKIMU 25 ZA UMWAGILIAJI ZA ASILI ZITAKAZOENDELEZWA MWAKA WA 2007/2008

S/N	KANDA	WILAYA	SKIMU	ENEQ (Ha)
1	Mbeya	Mbozi, Mufindi, Mpanda Iringa (V) Mbarali Ileje	Naming'ongo Mgololo Uruira Pawaga Lwanyo Chitete	1,000 500 500 500 500 250
2	Manyara	Kondoa Babati	Kisese Kisangaji	2,000 500
3	Mwanza	Magu Misungwi Kishapu	Mwamibanga Mbarika Ngeme	800 50 500
4	Kilimanjaro	Karatu	Karatu	1,450

		Same Same Monduli	Gonja Makanya Mto wa Mbu	1,200 600 600
5	Tabora	Kasulu Kigoma (R) Kasulu Kibondo Igunga	Titye Kashagulu Rungwe Mpya Katengera II Majengo	500 800 500 200 500
6	MtWARA	Mbinga Kilwa	Masepe Maruji	500 500
7	Morogoro	Ulanga Rufiji Mkuranga	Minepa Nyamweke Kisere	600 600 500
JUMLA				16,150

Kiambatisho Na. 8

MABWAWA 16 YATAKAYOJENGWA KATIKA MWAKA 2007/2008

S/N	KANDA	MKOA	WILAYA	SKIMU	ENE O (Ha)
1	Manyara	Singida	Manyoni	Msemembo	200
				Saranda	200
		Manyara	Mbulu	Dongobesh	200
		Dodoma	Mpwapwa	Msagali	200
2	Mbeya	Iringa	Kilolo	Dabaga	200
3	Mwanza	Mara	Bunda	Kisangwa	650
				Migungani	40
			Serengeti	Mesaga	350
			Tarime	Rwang'enyi	170
		Mwanza	Kwimba	Mahiga	200
		Shinyanga (R)	Shinyanga (R)	Bukigi	200
			Maswa	Nyida	200

4	Kilimanja ro	Tanga	Muheza	Misozwe	60
5	Tabora	Tabora	Sikonge	Isikizya	50
			Uyui	Usoke	300
			Urambo	Ulyanyama	500
JUMLA					4,085

Kiambatisho Na. 9

MABWAWA 9 YATAKAYOFANYIWA UPEMBUZI YAKINIFU NA KUSANIFIWA KATIKA MWAKA 2007/2008

S/N	KANDA	MKOA	WILAYA	SKIMU	ENEQ (Ha)
1	Mbeya	Mbeya	Mbarali	Umrobo	1,000
				Salimwani	500
				Kimani	700
				Lwanyo	600
			Kyela	Ngana	630
2	Mwanza	Mwanza	Magu	Simiyu	6,000
3	Tabora	Tabora	Nzega	Mihama	120
				Udushi dam	250
		Kigoma	Kibondo	Kasuga	50
				Nyambioka/Itumbiko	300
JUMLA					10,150

Kiambatisho Na. 10

**SKIMU ZA UMWAGILIAJI ZITAKAZOFANYIWA
UPEMBUZI YAKINIFU NA USANIFU WA AWALI
MWAKA WA 2007/2008**

S/Na.	Skimu	Wilaya	Eneo
1.	Kinyanyere	Bunda	400
2.	Lwambu	Bunda	250
3.	Muranda	Bunda	200
4.	Kirogo	Tarime	250
5.	Nyathorogo	Tarime	300
6.	Sumve	Kwimba	400
7.	Runele	Kwimba	400
8.	Nyamilama	Kwimba	300
9.	Mwanangwa B	Misungwi	350
10.	Ngh'ongh'oli	Misungwi	1,000
11.	Misasi	Misungwi	1,500
12.	N'hende	Misungwi	600
13.	Kafunzo	Sengerema	300
14.	Kasela	Sengerema	100
15.	Mashegesha	Maswa	1,000
16.	Chuganguni	Maswa	2,000
17.	Nyasisi	Maswa	500
18.	Ngulyati	Bariadi	1,000
19.	Nyaisenga	Bariadi	700
20.	Kasoli	Bariadi	700
21.	Kijongo	Kishapu	400
22.	Bulekela	Kishapu	1,350
23.	Nyenze	Kishapu	450
24.	Tindeng'hulu	Shinyanga (R)	400
25.	Singita	Shinyanga (R)	1,400
26.	Buhangaza	Muleba	80
27.	Buyaga	Muleba	40
28.	Buchurago	Bukoba (V)	400
29.	Kyaka kera	Bukoba (V)	500
30.	Kajunguti	Bukoba (V)	1,500
31.	Ushuhuda Group	Karagwe	500
32.	Mwisa Valley	Karagwe	150
33.	Ruguzye	Kibondo	250
34.	Luiche	Kigoma	5,000
35.	Madibira	Mbarali	3,600
36.	Kishisha	Siha	65
37.	Mbaghai	Korogwe	800
38.	Losimingiro	Monduli	350
39.	Lawate (dam)	Siha	160

40.	Usunga 1	Sikonge	300
41.	Shella	Urambo	100
42.	Kasimana	Uyui	150
43.	Mgondo gondo	Kibondo	500
44.	Kahama Nkalanga	Nzega	500
45.	Igurubi	Igunga	350
46	Sigili	Nzega	4,500
47	Lyamalagwi	Nzega	3,000
48	Mgambazi (V)	Kigoma (V)	1,000
49.	Luguvu	Kigoma (V)	1,200
50.	Machazo	Kigoma (V)	1,000
52	Katunguru	Sengerema	200
53	Kasela	Sengerema	100
54	Kalebezo	Sengerema	100
55	Mlela	Iramba	300
56	Mgungira	Singida (V)	1,050
57	Ulindwanoni	Nzega	250
58	Uywili	Nzega	300
59.	Mkowe	Ruangwa	320
60.	Mchomoro	Namtumbo	175
61	Lelolelo	Tunduru	150
62	Mavuji	Kilwa	1,500
63	Matandu	Kilwa	300
64	Nhobola	Kishapu	1,190
65	Kolandoto	Shinyanga	400
66	Seseko	Shinyanga	400
67.	Mwamashere	Shinyanga	600
68.	Usule	Shinyanga	250
69.	Simiyu	Maswa	900
70	Mwabaganda	Maswa	1,200
71	Budekwa	Maswa	680
72	Mwanangwa	Misungwi	500
73	Nyashishi	Misungwi	500
74	Durumwa	Maswa	1,500
75.	Luhala	Kwimba	500
76.	Ngudulugulu	Kwimba	600
77.	Welamasonga	Kwimba	400
78.	Bunyagongo	Mulebu	150
79.	Ibanda/Igaka	Geita	650
80.	Isima	Geita	240
81	Isanga	Kwimba	2,000
82	Mahenge	Kilolo	5,000
83	Biharamulo	Biharamulo	3,000
84	Nkono-Ikamba	Bukoba	8,000
85	Magogo	Kwimba	3,300

JUMLA	78,950
--------------	---------------

Kiambatisho Na. 11

**SKIMU ZA UMWAGILIAJI ZITAKAZOFANYIWA
 UPEMBUZI YAKINIFU NA USANIFU WA KINA MWAKA
 2007/2008 KATIKA KUTEKELEZA AGIZO LA RAIS LA
 KUUFANYA MKOA WA MOROGORO KUWA GHALA
 LA TAIFA LA NAFAKA**

S/Na	JINA LA SKIMU	WILAYA	ENEQ (ha)
1	Mbarangwe	Morogoro Vijijini	1,000
2	Mbwade		3,000
3	Bonye		5,000
4	Mngazi		700
5	Msonge		435
6	Milengwelengwe		100
7	Mgogoni		500
	Wami Luhindo		1,400
JUMLA NDOGO			12,135
1	Kidete/Mwasa	Kilosa	1,215
2	Kisiwani?Kilangali		1,253
3	Mlegeni		1,550
4	Msowero/Msolwa		1,880
JUMLA NDOGO			5,898
1	Itete	Ulanga	1,000
2	Ihowanja		1,700

3	Kivukoni		500
4	Lukande		480
5	Sofi Majiji		500
JUMLA NDOGO			4,180
1	Kiberege	Kilombero	200
2	Sululu		210
3	Kilama		210
4	Ikule		246
5	Maki-Sonjo		210
6	Udagaji		210
JUMLA NDOGO			1,286
1	Hembeti	Mvomero	3,500
2	Mbogo		351
3	Digoma		250
4	Lukenge		200
5	Vikenge		250
6	Mbugani		200
7	Tchenzema		300
8	Msufini		600
9	W/Dakawa		1,029
10	Mkata		200
11	Dihinda		500
12	Tangeni		200
13	Pinde		300
14	Mlali		1,000
15	Bunduki		500
JUMLA NDOGO			9,380
JUMLA			32,879

Kiambatisho Na. 12

MALENGO YA UZALISHAJI MAZAO MAKUU YA BIASHARA

Zao	Utekelezaji 2006/07 (Tani)	Malengo 2007/08 (Tani)
Pamba	130,565	300,000
Tumbaku	65,299	80,000
Chai	34,064	36,000
Kahawa	48,869	52,000
Pareto	1,500	2,200
Mkonge	30,934	46,000
Korosho	92,232	141,000
Sukari	192,535	312,000